
RIWAYA YA KIPELELEZI
MAYA
ABYAS
WA
MZIGUA
ULAYA

# MAYA WA ULAYA

Abyas Mzigua

2023

# NENO LA MWANDISHI:

Hongera kwa kuiweka kazi hii mikononi mwako. Hii ni riwaya iliyoandikwa katika dhamira ya kipelelezi. Wahusika, matukio na majina ya maeneo, vyote ni vitu vya kubuni tu. Haviingii katika uhalisia wowote. Huu ni utundu tu wa kifasihi, wenye dhima ya kufikisha ujumbe na burudani kusudiwa.

ABYAS MZIGUA
DAR ES SALAAM, TANZANIA
WHATSAPP: 0688589070
EMAIL: abyasmzigua@gmail.com

# 1

*"Gereza nililopo ni gereza la mwili tu, lakini fikra yangu iko huru zaidi ya kinywa cha muumini mbele ya Mungu wake katika maombi ya shida. Ukitoka hapa, nenda kairekebishe orodha yako ya vitu unavyoviogopa kupitiliza duniani, na namba moja uiweke akili ya binadamu isiyo kifungoni..."*

**Anza!**

Jalada la kesi ambalo lilikuwa mkononi mwake, ndilo lililomfanya Inspekta Kashmiri Kashmiri kuwahi kazini. Hakuwa na ratiba ya kufika mapema katika ofisi yake kwa siku hiyo, kutokana na aina ya majukumu yake ndani ya jeshi la polisi, ambayo pia humfanya mara nyingi awe nje ya ofisi. Majukumu ya upelelezi.
Kesi ngumu ambazo zingehitaji askari mgumu mwenye roho nzito katika ufuatiliaji, vinywa vya wakuu wake wa kazi vingelitanguliza mbele jina lake. Kama

ilivyokuwa kwa kesi hiyo, ambayo, hakutamani kuishughulikia, ila sifa zake ndizo zilizofanya akapigiwa simu harakaharaka usiku wa jana yake na kuelezwa kuna faili ambalo angepaswa kulipitia, na pale ambapo ingefika saa mbili kamili asub

uhi, awe ameingia ndani ya chumba cha mahojiano na mtuhumiwa. Ilikuwa ni amri kwake ambayo alitakiwa kuitekeleza.

Saa iliyokuwa ikimtazama juu ya meza yake, iliendelea kukatiza mitaa ya dakika na kunadi kuwa zimebaki kumi pekee ili muda wa kuingia ndani ya chumba cha mahojiano uwe umefika.

Alikuwa juu ya kiti kile alichokuwa amekikalia tangu saa kumi na moja alfajiri, akizipekua kurasa tano za kesi husika. Kwa mara zote aliporudia kukisoma kilichoandikwa, moyo wake haukuwa ukiamini.

"Haiwezekani..."Alijikuta akikataa kwa kujizungumzisha huku mkono wake ukivuta kahawa iliyokuwa imekwisha kupoa.

"...Ni binti mdogo sana huyu!" Aliendelea kuongea wakati huo kile kikombe kikiwa tayari kimeukaribia

mdomo wake. Akainamisha uso ainywe. Miwani iliyokuwa katika macho yake ikataka kuteleza. Haraka akaidaka kwa mkono wa kulia, wa kushoto bado ulikamata kile kikombe. Hakuinywa tena ile kahawa. Akaweka chini kikombe na kutazama saa yake. Zilibaki dakika tatu.

Alilifunga lile faili na hakuinuka nalo. Akachomoka ofisini mwake, akatembea kwa mwendo wa hatua thelathini na nane. Mpaka alipofika nje ya chumba ambacho kwa juu kuliandikwa maneno ya kiingereza. 'Interrogation room'.

Nje palisimama mtu. Aliye ndani ya sare za kipolisi pia, kama ilivyokuwa kwake. Mtu huyu alikuwa mfupi zaidi yake na mnene, alimpigia saluti. Alikuwa mkubwa wake wa kazi.

"Uko tayari Inspekta?" Mkubwa akauliza wakati Inspekta ameshika kitasa akiingia ndani.

Inspekta Kashmiri Kashmiri alishusha pumzi zake kwa nguvu na kujibu, "Nipo tayari!"

Akaruhusiwa aingie.

Ndani hakukuwa na mtu mwingine, zaidi ya viti viwili vilivyokuwa vimekaribiana, zilisalia nukta chache mno

vigusane. Akaketi katika kile kimoja. Kingine akakisogeza mbali kidogo kwa mguu wake. Kisha akatupa jicho katika dirisha lililokuwa upande wa kushoto na kuteremsha kichwa chake kutoa ishara.

Ni dirisha lisiloonesha kokote. Ukiwa ndani ya chumba hicho huwezi kumuona aliye nje. Dirisha hilo hutumiwa zaidi na wale wenye kuhitaji kuyafuatilia mahojiano wakiwa nje ya chumba. Yeye ni mzoefu wa kazi iliyokuwa mbele yake, na alikuwa na uhakika kuwa wapo waliokuwa wakimtazama. Alipokishusha kichwa chake kuitoa ile ishara, alimaanishwa yuko tayari na mtuhumiwa anaweza kuletwa!

Mlango ukafunguliwa. Akageuka kutazama ili kuthibitisha kile kitu cha ajabu kilichokuwa kwenye faili ikiwa ni cha kweli. Polisi wawili waliingia. Wakiwa wamekamata mitutu. Katikati yao alisimama mtuhumiwa ambaye mikono na miguu yake imefungwa. Huyu mtuhumiwa ndiye macho ya Inspekta Kashmiri Kashmiri yalitaka kumshuhudia.

Alikuwa ni binti. Binti mdogo sana. Sura yake ndiyo ileile ambayo ilikuwa katika picha iliyomo kwenye faili. Ndiye mtuhumiwa ambaye Inspekta Kashmiri Kashmiri

alitakiwa kwenda kumfanyia mahojiano. Faili la kesi likimzungumza kama binti wa miaka kumi na sita pekee.
Polisi walimfikisha mpaka kilipo kile kiti kilichokuwa mbele ya Inspekta Kashmiri Kashmiri, wakamketisha. Uso wa binti haukuwa katika hisia zozote za woga wala hofu. Hili lilimfanya Inspekta Kashmiri Kashmiri aendelee kustaajabika. Wakamfunga minyororo iliyokuwa kwenye miguu yake katika miguu ya kiti kile, mikono wakaizungushia mgongoni. Nayo waliifunga. Kisha polisi wakatoka nje ya chumba na kuwaacha wao wawili pekee. Binti mtuhumiwa na Inspekta wa polisi ambaye bado alikuwa ndani ya bumbuwazi kwa kile alichokuwa akikitazama.
Uso kwa uso. Inspekta alimtazama machoni, binti naye akamkazia ya kwake. Wakabaki wakikodoleana kwa urefu wa sekunde kumi. Ghafla, binti akaanza kucheka. Kicheko cha kulegea kabisa!
Ilimuwia vigumu Inspekta Kashmiri kujikaza, naye mbavu zake zikalegea wakaungana katika mtikisiko huo wa bandama. Wote wakacheka.

"Unacheka nini Maya?" Inspekta alivyoona imetosha, akauliza swali.

"Ni swali ambalo hata mimi napaswa kukuuliza Inspekta!" Maya alijibu. Jibu lililompa nafasi Inspekta, nafasi ya kuhakikisha sauti ya mtuhumiwa ni ya binti mdogo. Iliendana na umri ulioandikwa katika faili. Miaka kumi na sita.

"Haujashangaa nimelijuaje jina lako?" Inspekta Kashmiri Kashmiri alishusha swali la pili, lengo lililokuwa ndani yake ni kuipima akili ya binti huyo ambaye alimuita kwa jina la Maya.

"Hapana. Kama wewe vile ambavyo haujashangaa. Nimekuita Inspekta, na leo nd'o kwanza tunaonana!" Maya alizungumza kwa kujiamini. Binti hakutetereka.

Inspekta Kashmiri Kashmiri akajiweka sawa katika kiti. Kauli timamu ya binti yule mdogo ilijaa mantiki yaliyoweza kumtikisa.

Lakini bado alitaka kuonesha hakuna kilichoharibika na kila kitu kiko sawa, akamuuliza tena, "Enhee, niambie Maya. Umejuaje mimi ni Inspekta?" Ulimi wa Inspekta Kashmiri Kashmiri ulijaa ulaini kama baba anayezungumza na binti yake wa mwisho.

"Ni kweli silifahamu jina lako, lakini sare ulizovaa zenye mawe mawili katika mabega,  hicho ni cheo cha tisa katika mfululizo wa vyeo vya kipolisli. baada ya kutoka ASP, unakuja wewe...." Maya alizungumza usoni mwake akiwa ametapakaa tabasamu. Hakuwa na walau tone la hofu binti huyu.
Sasa Inspekta Kashmiri Kashmiri akaingia uthibitisho kuwa yule aliyekuwa mbele yake, udogo wake ulikuwa ndani ya umri tu. Na yale ambayo aliyasoma kwenye faili, kwa hakika ni ya kweli.
"Kwanini unaua?" Inspekta Kashmiri, rasmi akaingia katika mahojiano.
"Nadhani hili ni swali ambalo wale niliowaua walipaswa kulijibu. Kwa bahati mbaya, marehemu hazungumzi Inspekta..."
Jibu la yule binti likamfanya Inspekta Kashmiri Kashmiri ainuke kutoka kitini na kumsogelea mtuhumiwa. Kisha akatazama kule katika dirisha ambalo alitambua bila shaka walikuwepo wenye kufuatilia mahojiano yale.
"Maya, unajua kwamba ukitupa ushirikiano ndiyo utatoka humu ndani? Ukiwa mbishi, ukiwa mkaidi,

utafia humu humu. Unalijua hilo?" Inspekta Kashmiri alikuwa karibu na yule binti na kumzungumzisha kwa sauti ya chini yenye unyenyekevu.
Maya akamjibu, kwa sauti ya chini, kama ile aliyokuwa akiitumia Inspekta, "Gereza nililopo ni gereza la mwili tu, lakini fikra yangu iko huru zaidi ya kinywa cha muumini mbele ya Mungu wake katika maombi ya shida. Ukitoka hapa, nenda kairekebishe orodha yako ya vitu unavyoviogopa kupitiliza duniani, na namba moja uiweke akili ya binadamu isiyo kifungoni..."
Maya alizungumza kwa urefu na majivuno ya hali ya juu kwa yale aliyokuwa akiyatamka.
Hili likamfanya Inspekta arejee nyuma kidogo na kumtazama kwa makini binti huyo.
"Inspekta. Nimebakiza watu watatu ambao natakiwa niwaue. Wawili utawaua wewe. Mmoja atakayebakia, ni wewe ndiye utakayenifuata humu gerezani, utanitoa ili nikammalizie. Baada ya hapo, mtaamua wenyewe cha kunifanya!" Maya alizungumza kuhusu mauaji kama kwamba ni kitu cha mchezo.
Inspekta Kashmiri Kashmiri alikerwa na lile, akamsogelea pale karibu na kuanza kumkaripia, sauti

ya chini haikuwa rafiki tena! "Binti! Hili ni jeshi la polisi! Hii ni serikali. Umo humu ndani kwa kuua watu watano. Umeua viongozi wa serikali yenyewe! Umeua raia wasio na hatia. Unahojiwa, unaleta dharau. Unahisi wewe ni nani? Wewe ni nani hasa mbele ya sheria labda!!!?"

Uso wa Inspekta Kashmiri ulibadilika ule weupe wake na kuwa mwekundu shauri ya hasira; wa Maya ndiyo kwanza uliingia kwenye dimbwi la tabasamu la furaha.

"Usijali Inspekta. Kuanzia leo. Punde tu, baada ya kutoka humu, utanijua mimi ni nani. Wala haitachukua muda sana."

Mara mlango ukafunguliwa. Polisi waliingia. Mwisho wa mahojiano yale ulifika. Muda ulikwisha. Polisi walifika na kumnyanyua yule binti na kumtoa. Kabla ya kufikishwa mlangoni. Mtuhumiwa yule akamgeukia Inspekta na kumuita...

"Inspekta, nimesahau. Huko utakakokwenda kuanzia leo, najua tu utalazimika kunitafuta. Ukiulizia Maya utanikosa. Malizia wa Ulaya inspekta. Maya wa Ulaya. Sawa?"

Mlango ukafungwa na Inspekta Kashmiri Kashmiri kubaki mwenyewe ndani ya chumba kile kidogo. Alimsikia yule binti, lakini hakumtilia maanani kwa kudhani ni aina ya watuhumiwa walewale ambao siku zote amekuwa akikutana nao. Aidha kwa kujichetua, ama akili kuwaruka kweli.

Kwa vyovyote ambavyo ilivyo ama ingekuwa, wewe shikilia hayo maneno mawili tafadhali.....

Kwa kudhani!!

# 2

*"...tafsiri sahihi ya tusi, ni neno lolote lile lisilompendeza yule anayetamkiwa. Sipaswi kumshangaa anayesifiwa kwa kutukanwa na bado akadumu ndani ya kicheko!"*

Hii sura ya pili!

Imani yake, kila kitu duniani kimeumbwa kutokana na kanuni, na mambo yote huendeshwa kwa kanuni. Kanuni zinapovunjwa ama kukosewa ndiyo mwanzo wa kufeli kwa vitu vingi katika ulimwengu huu. Hivyo mara zote amekuwa ni muumini wa kanuni za eneo ama chochote kile akifanyacho.

Labda anaweza kuhukumiwa kuwa ni askari polisi ndiyo maana yuko hivyo. Lakini ni mara ngapi tumeshuhudia watu aina yake wakizibomoa kanuni hizo bila wasiwasi, tena hadharani, wakiwa ndani ya sare walizolia viapo vya utii?

Itoshe kutamkwa kwamba Inspekta Kashmiri Kashmiri ni askari muadilifu. Mwenye kupenda taratibu zifuatwe. Na hali inapokuwa kinyume chake, hugeuka kiumbe mwingine kabisa!!

Aliketi kwenye kiti kilichokuwa mbele ya meza. Hakuwa ofisini mwake. Baada ya kutoka kule kwenye chumba cha mahojiano, alielekea moja kwa moja katika ofisi ya mkubwa wake. Kuna jambo lilitokea, hakulielewa na alihitaji maelezo ya kutosha kabla ya kutenda lolote lile.

Baada ya dakika tatu, mlango ulifunguliwa na mkubwa wake aliingia akiwa ameongozana na mwanadada pembeni yake. Inspekta Kashmiri Kashmiri alimtazama kidogo msichana huyo, kuanzia chini, miguu yake yenye umbo mithili ya chupa zilizozowea viganja vya walevi, kigauni chekundu kilichokuwa kikiishia chini ya magoti, na mwendo wake wa madaha mithili ya paka aliyekosa chakula tangu usiku wa juzi, vyote hivi viliuteka umakini wa Inspekta Kashmiri kwa sekunde tano kabla ya kukaa sawa baada ya mkuu wake kumfikia karibu na kukumbuka ni wajibu wake kuinuka ili apige saluti. Akafanya hivyo haraka sana. Kisha

akarudi kuketi baada ya kuruhusiwa. Yule msichana naye akaja kuketi katika kiti kilichokuwa kikitazamana na kile alichokuwa amekalia Inspekta. Walielekeana lakini hawakuangalia. Inspekta alikuwa akimpa macho mkubwa wake akipatafuta pa kuanzia.

"Mkuu, samahani, kuna jambo nahitaji kujua..." Akapapata.

"Jambo gani, kuhusu huyu mgeni wetu?" Mkuu akajibu kwa bashasha na kuonesha mkono kwa yule mwanamke. Mnyooshewaji naye akajikomba kwa kujichekesha.

"Hapana. Sio. Kuna jambo limetokea kule Inte..."

Kabla hajamaliza..

"Oowh, nooo Inspekta! Noo! Umesahau?" Mkuu alimuingilia na kumkatisha huku akiminya macho yake na kumtazama Inspekta kisha yule mgeni kwa zamu kama vile alikuwa mwenye kuwafananisha, "Usiniambie umesahau Inspekta! What happens in the interrogation room, stays in the interrogation room! Rule number one! Umesahau Inspekta?" Mkubwa akakumbusha kuwa, chochote kinachotokea ndani ya chumba cha mahojiano ya kipelelezi, kinabaki ndani ya

chumba cha mahojiano ya kipelelezi. Hakipaswi kutoka nje, na hiyo ni sheria namba moja.

"Najua. Lakini mpaka nazungumza hili, tayari kuna sheria mmezivunja na sielewi ni kwa misingi gani mmezivunja sheria hizi!" Inspekta Kashmiri hakuhama kwenye mstari, pamoja na kukumbushwa kuwa yale anayotaka kuyazungumza hayapaswi kutolewa nje.

"Ins..." Mkuu akataka kuongea. Inspekta akaingilia...

"Mimi siwezi kuendelea na huu upelelezi mkuu. Mtuhumiwa anaingizwa chumbani, anafungwa mikono na miguu. Hii ni kinyume na sheria kabisa! Ndani ya chumba hamkuweka meza. Hamkunipa muda wa kutosha, mnanikatia mahojiano. Na mnafahamu kabisa sheria ziko wazi. Mimi niliye ndani ya chumba, kama nilivyosema kuwa niko tayari kufanya mahojiano, basi ndiye niliyepaswa kusema na kutoa taarifa kuwa mahojiano yamefika tamati. Sio ninyi. Sioni muendelezo mzuri katika hili na naomba nijitoe!" Inspekta Kashmiri Kashmiri alishamaliza kuzungumza hayo na kuinuka juu. Hayakuwa maongezi mabaya kwani vyote alivyovitamka, vilikuwa ndani ya sentensi halali kikanuni.

Mkubwa wake aliendelea kumtazama kwa muda, bila kusema neno. Anamfahamu Inspekta Kashmiri Kashmiri. Mtu wa misimamo. Na akiamua jambo nd'o ameshaamua.
"This is an order Inspekta! Na unalofanya ni kinyume cha utii! Disobedience!" Mkuu akajaribu kumuingizia hoja. Yule mgeni alibaki kimya tu, ameinamia. Alitamani walau kuitoa simu yake ili azuge kuwa anaitumia. Lakini ilikuwa ni kitu cha kwanza kukumbushwa kukizima alipofika tu getini. Akabaki akiutazama mguu wake na kuupekua mithili ya mnunuzi mpya wa simu katikati ya mji.
"Kwa hizi sababu nilizozitoa, niko tayari kupokea adhabu yoyote ile ikiwa nitaonekana nina makosa!" Kashmiri alizungumza kwa ukakamavu na kugeuka nyuma. Akaanza kuondoka.
"Inspekta...." Mkubwa alimwita, Inspekta akasimama kusikiliza, alirejesha uso wake na kutazama kule alikotokea,"Huyu ni mwanasaikolojia maarufu nchini. Mtaalamu pia wa masuala ya afya ya akili. Rehema Kagame!" Utambulisho wa mgeni ukafanyika.

Inspekta akamrushia tabasamu yule msichana aliyekuwa amekwishaionja ladha ya uthabiti wake walau kwa uchache kupitia mazungumzo yaliyokuwa yametokea, binti naye akajilazimisha kuonesha meno yake.
"Nice to meet you Rehema!" Inspekta aliongea hivyo kisha akatoka nje ya chumba. Mtu aliyetambulishwa kwake hakuwa na maana tena. Kesi alishaiangusha. Hakutaka kushughulika nayo.
Akaenda ofisini mwake. Mafaili mengi yaliyokuwa juu ya meza yakamlaki. Moja tu ndilo lililokuwa limemnunia. Faili la kesi ya Maya. Naye hakulijali. Akalichukua na kuliweka kando. Akaendelea na mambo kadha wa kadha aliyoamini ya muhimu zaidi. Alitaka kuyahitimisha kwa muda mchache kisha atoke akaendelee na majukumu mengine. Lakini mamlaka yaliyokuwa juu yake hayakuliruhusu hilo. Ndani ya lisaa limoja aliletewa barua yenye maelezo ya kutosha kuwa ameacha kesi aliyopewa kuipeleleza, kwa makusudi. Na alitakiwa kutandika saini yake kuithibitisha shutuma hiyo!

Kila alipopapasa kwa macho yake kutazama ikiwa kuna mahala pameandikwa zile sababu zilizomsababisha aikatae kesi hiyo, hakuziona. Akapotezea na kuweka uthibitisho wake wa wino. Alijua tu angeitwa mbele ya jopo la viongozi kuhojiwa. Na mara zote huwa kuna rekodi za video zinazochukua mahojiano. Aliamini rekodi hizo zingesimama kama shuhuda wake wa mwisho kwa yale ambayo angekwenda kuyazungumza. Baada ya saa moja nyingine, kile alichokuwa akikitegemea kikatokea. Maswali mazito mazito yenye lawama yalimshukia. Akapewa na onyo juu, lililobeba ahadi aliyotakiwa aisubirie. Kufutwa kazi!

Haikuwa mara ya kwanza Inspekta Kashmiri Kashmiri kuwaletea ukaidi viongozi wake. Hali yake ya kuwa mtu wa aiyepindesha mambo juu ya kanuni, aghalabu humtupa katika mikwaruzano ya kauli na viongozi waliokuwa juu yake. Huenda ndiyo sababu iliyomfanya akakosa kupandishwa cheo pamoja na uwezo mkubwa alionao. Achilia mbali uzoefu wa kudumu zaidi ya miaka mitano katika cheo hicho cha Uinspekta.

Cheo kilichokuwa kikimpa mshahara. Haukuwa mkubwa sana. Lakini ulimwezesha kuendesha familia yake, na kumiliki pia gari binafsi. IST toleo jipya. Ambalo kwa jioni ya siku hiyo, ndilo alilolitumia kuondokea ofisini kwake ili arudi nyumbani. Alichoka kwelikweli na alihitaji kwenda kupumzika. Hekaheka hazikuwa ndogo.

"Mimi nd'o maana hiki kitengo huwa sikitaki. Bora tu wanipange hata mfagia vyoo! Sheenzi!!" Alizungumza na kumalizia kwa tusi huku macho yake yakimakinika na barabara. "Ama kweli, tafsiri sahihi ya tusi, ni neno lolote lile lisilompendeza yule anayetamkiwa. Sipaswi kumshangaa anayesifiwa kwa kutukanwa na bado akadumu ndani ya kicheko!" Kisha akamalizia kauli hiyo kabla ya kuzishusha mboni zake katika 'dashboard' na kugundua mafuta pia hayakuwa katika kiwango sahihi cha kuikamilisha safari yake.

Mwendo wa mita kadhaa ukamruhusu akione kituo cha kujaza mafuta. Petrol station. Akakunja tairi zake na kwenda kuzisimamisha ili apate huduma hiyo.

Kitendo hiki kikamkera sana yule aliyekuwa akimfuatilia, akajikuta akibwaga sonyo zito. Naye

akaweka kituo kidogo kwa mbali, kumsubiri Inspekta aendeleze safari iliyokuwa na mwisho wenye kusudio la shari!!

# 3

*"...nyani mwenye busara, hawezi kwenda na wanawe katika shamba lililowahi kumtemea mlio wa gobole masikioni mwake!"*

Sura ya tatu.

"Mrefu, futi sita kwa makadirio, mwembamba. Ana mustach' ..."
"Ni huyo. Yuko umbali gani kutoka ulipo?" Simuni kuliuliza.
"Nimemfuatilia kote huko, na sasa ameshaingia ndani kwake, niko kwa maeneo ya nje ya geti la nyumba," alijibu kijana mweusi, mwenye mwili ulioshiba kwa mazoezi, huku akitazama kulia na kushoto kuhakikisha hakuna mabadiliko ya kuathiri harakati zake.
"Kwa sasa kazi yako isimamie hapo. Gwaya alishafika ndani tayari. Utasubiri kwa dakika kumi hapo nje. Hatuujui uwezo wa huyo Inspekta katika mapigano.

Zikizidi hizo, unaweza kuingia ili kuongeza nguvu." Maelekezo kamili yalitoka katika simu, na yule aliyekuwa akiyapokea akakubali na kuahidi utiifu.

Inspekta Kashmiri Kashmiri alishaliingiza gari lake ndani, kwa kujifungulia geti mwenyewe. Punde tu baada ya kulipaki. Macho yake yakakutana na maajabu ya kwanza. Tabasamu la mkewe!

Tabasamu lililokuwa limefutika kwa miezi kadhaa kwa visa visivyo na sababu wala maana, ugomvi wa kila leo, gubu na kususa kusiko na idadi. Inspekta Kashmiri Kashmiri alimsogelea mwanamke huyu na kumbusu katika paji, kisha wakatazamana kwa dakika kadhaa huku wakichekeana. Wakamalizia na utani wa Inspekta kulipapasa tumbo la mwanamke huyo. Sababu kuu ya kuvunjika kwa amani ya nyumba. Mke alikuwa na ujauzito mbichi.

"Kuna mgeni!" Mwanamke akatoa taarifa.

Ile bashasha iliyokuwa katika uso wa Inspekta ikaanza kupeperuka taratibu.

"Mgeni?" Inspekta akahoji kwa mshangao.

Mke akajibu kwa kukitikisa kichwa chake.

"Nani?" Inspekta aliuliza. Hakuwa akiutarajia ugeni kwa siku hiyo. Uwe wa kushtukiza ama kwa miadi. Mtu pekee aliyekuwa akiweza kufika nyumbani hapo bila taarifa ni mama yake kutoka mkoani Mwanza. Naye, safari yake ingeandamana na utitiri wa dalili. Mara amuulizie mkwe, anaendeleaje, kisha ahamie kwenye hali ya hewa, aje kwenye adha ya usafiri wa mji kama kwamba ni mtembezi. Ili mradi tu. Na haya yakiongozana kwa mfululizo wa wiki nzima, basi Inspekta Kashmiri Kashmiri angekuwa tayari kumlaki mama yake. Kwa siku hiyo ilikuwa tofauti. Hili likawa ajabu la pili ukiacha lile tabasamu la mkewe.

"Amesema ni rafiki yako wa shule ya msingi." Mke alijibu.

Shule ya msingi?

Inspekta alihitimu kiwango hicho cha elimu miaka zaidi ya ishirini iliyokuwa imekatika. Hakuwa akikumbuka hata muundo wa darasa ulikuwa vipi. Ni rafiki gani huyo wa shule ya msingi aliyejaaliwa kumbukumbu kali mithili ya wino wa dhahabu juu ya karatasi laini.

"Yuko wapi?" Inspekta aliuliza ili akamuone. Akajibiwa yuko varandani. Sebuleni. Akazichangamsha hatua zake kwa haraka bila kumakinika na lolote. Mara baada ya kuukaribia mlango wa kuingilia ndani, akapatikana wa kumzuia akiwa na bunduki mkononi. Ikaelekezewa katika nyama yake ya uso.
"Tulia!" Sauti ikamkoromea.
Mke wa Inspekta macho yamemtoka. Rafiki wa shule ya msingi aliyekuja kwa vicheko vingi pamoja na zawadi za kutosha mkononi, sasa ameshika bunduki kumuelekezea wa–ubani wake akiuhitaji utulivu.
"Naitwa Gwaya. Nipo hapa kwa jambo moja tu Inspekta. Moja pekee. Sina shida na wewe wala mkeo!" Mshika bunduki alinadi dhamira yake.
Inspekta kijasho kikaanza kumyemelea. Kijasho cha upande wa kichwa. Akajikomba kwa nguvu zilizokuwa zimesalia ndani mwake na kuhoji, "Jambo gani?"
"Nahitaji faili la kesi uliyokabidhiwa leo! Najua wewe ndiye mpelelezi wa kesi hii. Na bila shaka faili litakuwa ndani ya gari lako. Twende ukatutolee!"
Inspekta alilitambua lile lililokuwa likihitajika, faili la kesi ya Maya. Bunduki iko katika paji lake. Mkewe

machozi yanamtiririka pembeni yake. Mwanamke huyo ni sehemu ya furaha yake katika maisha yake. Hakutamani lile liendelee. Akajaribu kurudi nyuma kwa hatua kadhaa kwa kuigizia yuko tayari kulielekea gari. Kuna hesabu alitaka kuzipiga ili kuhakikisha ile bunduki anaidondosha kutoka katika mikono ya aliyeishika. Kabla hazijafikia katika kiwango cha ukamilifu, mkewe alikuja kwa kasi sana na kumfikia. Hili likabadilisha mkondo mzima wa tukio. Mvamizi aloyetambulisha kwa jina la Gwaya, alimkamata kwa nguvu sana mwanamke huyo na kumpiga ngumi bila kutazama ni wapi ilipokwenda kutua. Kisha akamsogeza karibu. Inspekta alipotaka kujitikisa tu kufanya maamuzi ya kumkomboa, bunduki ilishapata makazi mapya, makazi ya kwenye kichwa cha mwanamke huyo.

"Inspekta, nyani mwenye busara, hawezi kwenda na wanawe katika shamba lililowahi kumtemea mlio wa gobole masikioni mwake. Zichunge hatua zako, ubongo wa mkeo unaweza kusambaratika kwa mjengeo mdogo mno wa kidole changu cha shahada!"

Inspekta alitulizwa kwa mkwara mzito. Akawa mpole na asijue la kutenda kwa sekunde zile..
Kabla hajalipata, "Utatupa faili la kesi ama utatuachia mkeo?", aliulizwa.
Faili la kesi Inspekta alitolee wapi na alishajiengua?
Akaanza kujing'ata ng'ata huku akitafuta la kuongea ili aeleweke. Hajafanikiwa, yule aliyekuwa nje ya geti naye akazama ndani. Sasa wavamiwaji wakawa wawili, na wavamizi wakawa wanne walio na silaha. Mikono ya Inspekta ilipaswa ielee juu kwa muda wote. Alisogelewa na kupigwa mtama wa nguvu! Kisha akagongwa na kitako cha bunduki katika shingo yake, upande wa kushoto. Fahamu zikampotea na kumrejea pale ambapo ziliamua.
Akazinduka mkewe yuko pembeni, kilio cha uchungu kikayakithirisha mashavu yake machozi. Giza limeshatanda kuashiria usiku umezipiga hatua za kutosha. Inspekta baada ya kujikusanya na kukaa sawa. Macho yake yakakitana na michirizi ya damu katika nguo za aliyekuwa akilia. Alikurupuka.
"Mke wangu, nini? Nini tatizo?"
Mke ni kilio tu.

Inspekta akakamata simu yake haraka sana na kumvutia waya daktari. Daktari wa karibu. Ambaye aliiweka na kuitimiza ahadi yake ya kufika ndani ya dakika kumi. Huduma ikatolewa. Huduma ya kwanza. Kisha yakatakiwa kwenda kufanyika matibabu mengine hospitalini. Usafiri ukawa ni lilelile gari la Inspekta. Alimuwahisha mkewe katika kituo cha afya, kisha yeye akaelekea katika kituo cha karibu cha polisi ili kutoa taarifa, ulikuwa ni mwendelezo wa tabia yake ya kupenda kuzitii kanuni na kuufuata utaratibu. Halikuwa tukio jema, lakini walau uzima waliokuwa nao wote wawili ulimpa matumaini Inspekta huyu wa polisi.

Kurudi hospitali, akakutana na uso wa huzuni wa daktari. Uso ulionyong'onyea. Tumbo la mashaka likamtikisika.

Dakati vipi, mke wangu anaendeleaje?

Namna daktari alivyozishusha pumzi kabla ya kujibu, miguu ya Inspekta nayo ikatetemeka na kumfanya apepesuke. Akaomba waketi ili wazungumze. Daktari aliridhia na kumwambia waingie ofisini. Walikaa chini na kumpa maelezo. Maelezo yenye taarifa.

Kuwa, mke ni mzima kabisa wa afya, lakini kile kiumbe alichokuwa amekibeba tumboni, tayari kilishaipungia mkono wa kwa heri dunia na bado hakijaitembelea. Hili lilimsisimua mno Inspekta. Akatulizwa. Akaelezwa kuwa uimara wa mkewe umelala katika ukuta na msingi wa mapokezi yake. Hayupo mwingine zaidi wa kumuweka sawa mwanamke wake, zaidi ya yeye mwenyewe. Hivyo angepaswa kulifungasha tukio lile kwa ushupavu katika nyama za kifua chake. Asioneshe ni zito na kuhakikisha mkewe anaamini ni sehemu ya mipango ya Mungu isiyokuwa na mipaka katika kukamilika ama kutokukamilika kwake. Inspekta Kashmiri Kashmkri aliyapokea majukumu hayo. Akayapa uzito na kuzifikisha habari mpaka katika kituo chake cha kazi. Kituo kikubwa cha kati. Huko akapewa pole na likizo ya siku saba. Ili awe karibu zaidi na mgonjwa. Peke yake asingeweza. Akapiga simu nyumbani kwao. Kijijini Mwanza. Baada ya siku mbili, msichana, msaidizi wa kazi, akaletwa. Hii likampa upenyo kidogo Inspekta Kashmiri. Walau akaweza kutoka myumbani na kuzunguka maeneo jirani ili kuyapunguza mawazo. Kitendo cha mkewe kupoteza

ujauzito, kilikuwa kikimtafuna na kummumunya. Hakikuwa na malemgo ya kumbakiza. Hasira zilizokuwa zikimfukuta ndani kwa ndani hazikuwa katika uzani rahisi wa kulinganishwa na kitu kingine. Lilikuwa ni jambo alilolisubiri kwa miaka saba ya ndoa yake. Leo hii wanatokea tu watu kusipojulikana na na kumyeyushia ndoto zake za kuitwa baba.

Inspekta Kashmiri Kashmiri alikuwa ndani ya baa. Hanywi pombe. Aliwafuata tu marafiki ambao pia waliyaheshimu maamuzi yake. Hawakumshawishi. Akaketi pamoja nao katika meza moja wakitazama mpira. Wakati wenzake wakiendelea kuwalaumu wachezaji wa timu zao kwa kuvurunda uwanjani kama kwamba kule katika runinga walikuwa wakiwasikia, yeye kuna jina lilimuinua katika siti na kumfanya aage kurudi nyumbani. Moja kwa moja!

Baada ya kujitandaza katika kochi. Akalitafakari upya jina hilo.

Magwaya!!!

Hakuzingatia ni vipi linaandikwa lakini lilitamkika likisindikizwa na lawama za uzembe. Kwake jina hili

halikuwa na sifa hiyo kila alipoziondoa silabi mbili za mwanzo, na kubaki Gwaya.

Gwaya!

Jina la mvamizi mmojawapo. Lilirejea kichwani mwake na kujikuta akitamani kukilipa kisasi. Kwani tayari alikuwa na pa kuanzia. Kisasi cha kuondoshewa mtoto wake aliyekuwa amejijaza hamu kumsubiri.

Angempata vipi huyu Gwaya?

Haikuwepo njia nyingine zaidi ya kujirejesha upya katika mstari kesi ya Maya. Maya wa Ulaya!

Akachukua simu yake na kupiga sehemu. Hii, ilikuwa ni simu ya maamuzi.

# 4

Baba alimkimbia mama punde tu baada ya kugundua ni mjamzito. Kwa simulizi za wale waliofanikiwa kumuona mwanaume huyo, walisema alikuwa ni mtu mwenye asili ya India. Kuanzia ngozi hata kwa namna alivyokuwa akizungumza. Mama aliikuza mimba yake kwa tabu sana mpaka pale ilipokomaa. Kwenye kipindi chote hicho cha mateso, mwanamke huyo akajiapiza kutokupenda wanaume tena maishani mwake. Alijipa nadhiri kuwa, kama mwanaye aliye tumboni angezaliwa wa kike, basi angemweleza kutokuwapa imani wanaume. Ikibidi asije kukubali kuja kuishi na mwanaume maishani mwake kote.

Mungu si Athumani, anapanga kile akitakacho. Miezi tisa ikakamilika. Uchungu wa uzazi ukamvaa mwanamke huyu akiwa njiani katika harakati zake za kutembeza mboga za majani. Katikati mwa viunga vya jiji la Mwanza. Akadondoka chini na beseni lililokuwa

kichwa kujifunika mchanga. Michicha, matembeleo na kisamvu, zote zikalikumbatia vumbi.

Huku akipiga makelele, kundi la watu likamzunguka. Watu wengi. Wale waliokuwa wamejaaliwa upevukaji wa fikra, wakaanza kuandaa mazingira ya haraka. Watoto wakasogezwa mbali. Wanawake wenye kanga katika viuno vyao wakasaidia kuzitegua. Ukawekwa ukingo wa maana usioruhusu hata hewa kukatiza. Hii ilikuwa ni wodi ya uzazi ya dharura. Na kwa wakati huo, nusu ya wanawake waliokuwa eneo lile walijua nini kinatakiwa kifanyike. Sizungumzii hawa wapamba kucha wa miaka hii ambao kwa tukio hilo kila mmoja angehangaika kuitafuta kamera yake ya kwenye simu ili apate tukio la kupeleka kwenye mtandao wake wa kijamii. Hapa naigusa jamii ya kisukuma iliyokuwa haitamki neno lolote kwa yule mwanamke pale chini zaidi ya 'sukuma!'.

Mzazi kafunikwa kanga kwa juu. Yule mwenye utaalamu zaidi akawa chini akimstahi kwa aibu kubwakubwa anazokumbana nazo mzazi yeyote kipindi cha kutoa kiumbe tumboni mwake.

Jasho la maji lilishamtoka vya kutosha mzazi sasa lilisubiriwa la damu. Machozi yakamkauka. Maumivu aliyokuwa akiyapitia, akatamani na yeye ile mimba mapema angeikimbia.
Angekwenda wapi sasa na kuliacha tumbo lake?
Mimi na wewe hatujui kama walivyokuwa hawafahamu wale waliokuwa wamemzunguka mzazi ambaye tayari alishamtoa mwanadamu kamili mwilini mwake na fahamu kumpotea.
Ni nani huyu mwanamke? Ametokea wapi? Kuna anayemfahamu hapa?
Maswali yote hayo yalikosa majibu yenye msaada. Mzazi akawahishwa haraka katika kituo cha karibu. Ndugu wakatafutwa ili waje watoe msaada. Walipopatikana, hali zao zilikuwa ni za wao wenyewe kwanza kuanza kupewa msaada. Walikuwa hoi. Hospitali ikawasamehe. Baada ya siku kumi mzazi aliruhusiwa huku akiwa ameshapewa ubatizo wa jina la baba yake. Cashmir. Jina la baba liliandikika hivyo. Na pale lilipopokewa na ndimi za kibantu, lilipinduliwa vizuri kabisa. Likapambwa na kupendeza. Hatimaye likapatikana Kashmiri. Ukiongeza na ule ubini wake, ni

Kashmiri Kashmiri! Hata pale alipofika ukubwani, matukio yote hayo mama mtu alimsimulia mwanaye wa pekee. Kashmiri akaishi na hadithi hiyo huku akidhamiria kutorudia makosa aliyowahi kuyafanya baba yake asiyefahamu alipo! Labda ndiyo sababu iliyomfanya akamsubiri kiumbe kutoka katika tumbo la mkewe kwa hamu kiasi kile. Tena kwa subira ya miaka mingi. Halafu ghafla, ghafla, kisa faili la kesi, anatokea mtu mwenye jina la ajabu na kuiyeyusha ndoto hiyo!

Hapana. Aliamua kuchukua hatua ambayo aliamini ni sahihi zaidi.

Simu iliyokuwa sikioni mwake iliendelea kulalamika kuashiria kuwa huko inakopigwa inaita.

Inspekta Renatus!

Kwenye kioo cha simu kulisomeka hivyo mara baada ya kuitoa sikioni na kuiwekea kipaza sauti. Simu akaitua mezani. Ilivyopokelewa, akajipa mtulivu mwepesi na kuanza kuzungumza.

"Ni siku nyingi sana! Habari yako kiongozi?"

Kicheko hafifu na kifupi mno kikasikika katika simu, kisha kuitikiwa, "Salama kabisa. Mimi nilikueleza siku unaondoka. Dar Es Salaaam patakuteka. Hukutaka

kuamini! Ona sasa!!" Lafudhi ya mzungumzaji ilikolea usukuma.

"Ni kweli. Lakini hii simu haijawa kwa wema ndugu yangu!" Inspekta Kashmiri Kashmiri alizungumza kwa upole.

"Kwanini?" Alihoji kwa mshtuko Inspekta Renatus—simuni. Akauliza, "Nini tatizo ndugu yangu?"

Wawili hawa waliwahi kufanya kazi ya pamoja katika kituo kikuu cha kanda ya ziwa. Kabla ya Inspekta Kashmiri Kashmiri kutenda tukio la kiweledi lililomfanya asogezwe mjini. Dar Es Salaam. Ukaribu mkubwa waliokuwa nao kwa miaka hiyo, wakashibana kiasi cha kujihisi ni ndugu wa mzazi mmoja.

"Nimelazimika kurudi kwa Kaka Kubwa! Sijui nikueleze vipi. Lakini namhitaji Kaka Kubwa haraka iwezekanavyo!" Inspekta Kashmiri Kashmiri akaitandaza dhamira yake.

"Kaka kubwa? Hapana. Ndugu yangu, uko sawa kweli? Hapana kaka! Hapana!!!" Inspekta Renatus aligoma. Hakulitaka kabisa suala hilo.

"Si kwa jambo baya. Kuna jambo tu nahitaji anisaidie. Jambo moja pekee. Moja tu!!"

"Siwezi kukuruhusu ushirikiane na mtuhumiwa ndugu. Kaka kubwa ni ndugu yetu. Ni rafiki yetu, lakini ukumbuke tulikubaliana kumuacha na maisha yake. Ukumbuke!"

Inspekta Kashmiri Kashmiri akashusha pumzi. Kisha akajieleza kwa ufupi, "Ndugu yangu, samahani kwa kughafilika, sikukwambia. Labda ni kwa furaha kubwa niliyokuwa nayo baada ya kuligundua. Lakini, hatimaye shemeji yako alipata ujauzito. Hivi tunazungumza, yupo aliyempiga na kuufanya uharibike!"

Inspekta Renatus huko aliko akasikitika. Akakumbuka namna ndugu yake alivyoteseka kuhakikisha anapata mtoto. Ikabidi ahoji sababu ya namba ya Kaka Kubwa kuhitajika. Alipoelezwa, akawa hana namna zaidi ya kuitoa. Kisha akaomba kwa vyovyote vile, asihusishwe.

Ilipotumwa, muda huohuo, Inspekta Kashmiri Kashmiri akaitwangia. Simu ikapokelewa. Maongezi yakafanyika. Maongezi yaliyojaa masharti kwelikweli. Kisha ikahitajika safari ili yakawekwe makubaliano. Hayakuwa mazungumzo ya kukamilika kwa amani katika simu.

Ndege ya asubuhi na mapema ikamfikisha Inspekta Kashmiri Kashmiri ndani ya jiji la mawe. Mwanza. Mwenyeji wake aliyekuwa amezungumza naye usiku wa jana yake, akamweleza pa kumpata. Wakakutana. Makubaliano haramu sana yakafanyika. Inspekta Kashmiri Kashmiri hakuwa na namna nyingine zaidi ya hiyo.

Mtu aliyekutana naye alikuwa ni Kaka Kubwa. Hilo ni jina la utani tu, ambalo lilifahamika kulizidi lile la uhalisia. Huyu alikuwa ni mhalifu. Inspekta alikifuata kiatu cha baniani mbaya. Akaelezwa kuwa tiba anayotafuta, asubiri jioni ya kesho yake atapata majibu.

Kisha, ili kufuta ushahidi na dalili zozote zile za kugundulika ikiwa uchunguzi ungekuja kufanyika baadaye, akaenda kwenye kijiji cha mama yake na kusalimia. Alilala huko. Kesho yake asubuhi akaaga na kurejea nyumbani. Mjini. Akiisubiri jioni.

Unadhani ilikawia basi?

Kiza kikaingia. Saa moja, saa mbili, saa tatu.

Saa tano! Tano na dakika zake! Simu yake ikaita. Jina likiwa ni la mkubwa wake wa kituo. Taarifa ni kuwa,

askari aliyepewa kazi ya kuipeleleza kesi ya Maya, ametekwa na hajulikani alipo tangu usiku wa jana yake. Hivyo, kesi hiyo, pamoja na kesi ya Maya, zote zinapaswa ziwekwe mapema sana mkononi mwake. Akaulizwa ikiwa yuko tayari. Inspekta Kashmiri Kashmiri akaomba dakika chache za kutafakari.

Haikuwa kutafakari, bali ni kuandika tu ujumbe mfupi kwa Kaka Kubwa, "Hakikisheni anakula vizuri. Pia haumizwi!"

Simu ilipoonesha ujumbe umefika. Akaufuta na kumpigia mkubwa wake. Maneno matatu yakamchomoka kwa dhati kutoka katika uvungu wa moyo wake, "Niko tayari mkuu!"

# 5

Hatua zake zilipokuwa zikiinusa sakafu kuelekea ofisi yake ilipo, zilimeza harufu ya kisasi. Inspekta Kashmiri Kashmiri tayari alifika katika kituo cha kazi. Zile siku saba hazikuwa zim'esha. Lakini walau mkewe alipata ahueni ya kuweza kusimama na kupanda basi kwa ajili ya safari ya masaa kadhaa.

Ndiyo, alimpeleka mkewe kijijini kwa mama yake. Hakutaka kumuingiza katika hekaheka alizokuwa amedhamiria kuzivaa. Aliyahofia maamuzi ya wale wavamizi kujirudia. Wakaenda tena nyumbani kwake. Aliweka nia ya kuingia katika vita ya kuipigania damu yake iliyopokonywa uhai ikiwa bado iko tumboni.

Aliufungua mlango wa ofisi yake. Kisha akaenda moja kwa moja katika meza na kuliweka faili juu. Faili alilopewa na mkubwa wake wa kazi. Faili la kesi ya

binti mdogo, Maya. Inspekta hakumtaka yeyote ndani ya kesi hiyo zaidi ya Gwaya. Gwaya tu!

Mkubwa wake alimkabidhi karatasi. Akamhitaji aoredheshe mahitaji. Aandike vitu vyote anavyotaka kufanyiwa ama kupatiwa, ili kuleta ufumbuzi kwa kesi hiyo. Kitu cha kwanza kabisa, Inspekta aliomba aletewe Maya. Yule binti mtuhumiwa. Na hakumtaka kule katika chumba cha mahojiano, laa hasha. Alitaka msichana huyo apelekwe ofisini mwake, halafu waachwe wao wawili tu—wazungumze.

Alijiandaa katika kujieleza kwenye hilo. Hata pale ambapo angehojiwa kwa nini anahitaji kitu cha hatari kiasi hicho, tayari jibu lenye maelezo ya kunyooka lilikuwa kichwani mwake. Angesema anataka upatikane usiri. Angedai binti huyo mdogo uelewa wake ni mkubwa, na pemgine anafahamu mazungumzo ya kwenye chumba cha mahojiano huwa yanafuatiliwa. Hivyo, ili kumpa mtuhumiwa huyo uhuru, mahojiano yafanyike ndani ya ofisi yake. Hilo lilikuwa ni ombi la kwanza. La pili likawa ni silaha. Inspekta alihitaji kupatiwa bunduki. Apatiwe bunduki

ya kisasa yenye risasi za kutosha. Na hili la pili, litendeke baada ya la kwanza kukamilika.

Wakamtii. Hawakuwa na namna. Jukumu lililokuwa mbele yao lilikuwa ni zito. Asingekuwepo askari mwingine wa kuitatua kesi nzito kiasi kile. Hawakuwa na budi kukubali. Isipokuwa, lile la kubaki peke yake na Maya halikuwaingia akilini, wakamkabidhi kinasa sauti. Akiweke juu ya meza, mazungumzo yanapoendelea, wayasikilize huko waliko. Inspekta hakupingana nao.

Maya akaletwa. Akapelekwa mpaka kilipo kiti kilichopo mbele ya meza yake. Kisha askari wawili waliokuwa wameongozana na mtuhumiwa, wakatoka nje. Wakawaacha wao wawili tu: Inspekta Kashmiri Kashmiri na Maya. Maya akiwa hajafungwa mikono wala miguu. Kama alivyoagiza.

Ilikuwa ni tofauti na makutano yao ya siku ya kwanza.

Maya alimtazama kwa tuo Inspekta ambaye aliinuka na kwenda mlangoni.  Akaufunga ule mlango. Maya aligeuza shingo yake akimtazama kwa yote hayo. Mpaka alivyorejea katika kiti chake na kuketi.

"Maya," aliita Inspekta akivuta droo la kwenye meza yake na kutoa kisu. Akakiweka kwenye meza. "Kama ninakushangaza, basi nikiri kuwa ni kweli leo nimepanga kukushangaza."
Maya hakutia neno. Binti huyu mweupe, mwenye kila dalili za kuja kuwapigisha vikumbo wanaume ukubwani mwake, aliendelea kumtazama tu Inspekta Kashmiri Kashmiri.
"Maya, kisu hiki kilichopo mezani," akakiinua kwa mkono wake, "kitakata ngozi yako mdogo mdogo, ikiwa tu, utakataa kunijibu maswali yangu!"
Maya akacheka sana!
Inspekta akainuka. Akiwa amekikamata kile kisu, lengo ni kumfanyia kitisho tu binti huyo, wala hakudhamiria kumjeruhi. Lakini alipokea kile ambacho hakukitegemea. Binti alijichupa juu kutoka pale kitini na kupanda mezani kwa wepesi wa karatasi. Akakipiga teke kile kisu. Kulikuwa kuna chupa ya maji. Aliifungua kwa uharaka na kuimwagia palepale juu ya meza. Alikilowesha kile kinasa sauti. Halafu akarudi katika kiti na kujituliza kama vile hakuna kilichotokea.
Inspekta hoi! Ilikuwa ni kufumba na kufumbua tu!

"Nimefundishwa kutokumdhuru yule asiye na ubaya nami. Inspekta, nakushauri utumie njia za amani tu. Tuongee. Hakuna anayeweza kutusikia humu ndani. Hicho kinasa sauti ulichokabidhiwa, tayari kimeharibika. Naweza kukukaba, roho yako ikatoka taratibu mno katika mikono yangu na usipate wa kuja kukunasua!"

Inspekta Kashmiri Kashmiri akiwa amesimama, mabega yakamshuka akiendelea kumtazama yule binti.

"Wewe ni nani?" Ilibidi Inspekta ahoji. Ubishi wote ulimwisha. Ukaidi ulimepeperuka. Ukaidi wa kung'ang'ania Maya aletwe kwake mikono yake ikiwa huru, ulimtoa kijasho cha pua!

Maya kama kawaida yake, alicheka.

Kisha akajibu, "Muda tulionao hautoshi. Tayari tumeharibu kifaa chao. Hivi punde, watatuma timu ya dharura kuja humu ndani. Muda hauwezi kutosha nikitaka kukueleza ya muhimu. Ila, kuna...."

Ngo! Ngo! Ngo! Ngo!

Kabla Maya hajamaliza kuzungumza, mdomo wake ukakatishwa na mlio wa mlamgo uliokuwa ukigongwa. Mlango wa ofisi waliyomo. Yale aliyoyatamka Maya

hayakuchukua sekunde kutokea. Bila shaka ni kiumbe mwenye kuzifahamu vilivyo taratibu za kipolisi.

Ule mlango na kelele zake ukapuuzwa, Maya aliendelea, "Magomeni mapipa. Ukifika. Ulizia kaburi la Bibi Mboga!"

"Kaburi? Bi...!" Inspekta hakuelewa na kuingia kigugumizi.

Maya yuko makini na mlango huku akihakikisha anakamilisha maelezo yake kwa wepesi."Sina muda wa kukueleza hili Inspekta. Ulizia lilipo kaburi la Bibi Mboga. Ukimkuta, atakueleza kila kitu kuhusu mimi. Naamini utasaidika kwa vingi."

Bado mlango unaendelea kugongwa, "Unasema bibi nani?" Inspekta anauliza huku akielekea kule mlangoni.

Maya akamjibu, "Bibi Mboga!"

Inspekta akalinasa lile jina. Lakini maelezo kulihusu ndipo yaliendelea kumvuruga. Ameelezwa akalitafute kaburi, kisha azungumze na huyo aliyezikwa kaburini huko.

Ajabu ya kiwendawazimu! Mtu afunge safari akazungumze na kaburi!

Inspekta alishaufungua mlango. Timu ikamkagua Maya, ikamkagua Inspekta. Wote wako sawa. Kisha mtuhumiwa akatolewa katika ofisi ile. Inspekta Kashmiri Kashmiri akabaki mwenyewe. Baada ya dakika tano, mkubwa akaingia. Akihitaji maelezo ya kutosha kwanini kinasa sauti kilizimwa na Inspekta Kashmiri Kashmiri alikwenda kwa kukawia kuufungua mlango. Kuna nini?

Jibu rahisi kabisa likamtoka Inspekta, kwamba, allipokuwa akimtishia binti huyo kisu, akajikuta anakwaa maji yaliyokuwa kwenye chupa na yakamwagikia kwenye meza. Mahala kilipokuwepo kinasa sauti. Na kuhusu kukawia kufungua, akahamisha lawama hizo na kuzirejesha kwao, akidai wamejisahau na kulirudia kosa lao lilelike la kupangiana muda wa mahojiano. Mkubwa akakosa la kushika kujitetea na Inspekta Kashmiri kuwa mshindi. Wakapeana pole na kutakana radhi. Siku ikaendelea, Inspekta Kashmiri Kashmiri hatutaka kulaza damu. Aliondoka ofisini na kufunga safari mchana wa siku hiyohiyo kwenda Magomeni Mapipa. Kule alipoelezwa. Akasogea mpaka kilipo kijiwe cha bodaboda, akalipaki

gari lake na kushuka. Kila aliyemkurubia kumuuliza kuhusu jina lile, Bibi Mboga, hakuna ambaye alithubutu kumjibu. Wengine alipowafuata na kuwatamkia jina hilo, waliwasha vyombo vyao na kukimbia. Yule aliyekutana naye, uso wake ukiwa ndaninya bashasha, angelitaja tu jina hilo, wajihi wake ungekumbatia nyama kwa makasiriko na kuzichakata hatua zisizomruhusu kugeuka nyuma.

Bibi Mboga ana nini?

Ghafla, akiwa ameegemea gari, ubongo umezama ndani ya fikra za kukata tamaa ama kufanya uamuzi mwingine, akakatiza mbele yake kijana ambaye alibeba mzigo mkubwa wa makopo ya plastiki. Inspekta alipompa tu jicho. Akapata wazo. Akatumia nguvu ya ushawishi. Mzigo wote ule aliokuwa nao, aliupigia hesabu na kung'amua asingeweza kupata hata elfu tano. Inspekta akamtolea elfu ishirini na kumuulizia Bibi Mboga!

"Unaulizia Kaburi la bibi Mboga? Nifuate. Ni muda mrefu sana nimekua nikikusibiri Inspekta!" Yule muokota makopo akaweka zigo lake kando na kuongoza njia. Mwili wa Inspekta ukagawanyika.

Kipande cha juu kikiwa ndani ya bumbuwazi, huku miguu ikilazimika kuiunga safari ile yenye ufunguzi wa ajabu.
Maswali yakawa mengi na muda wa kubandikiwa majibu ulibaki mchache. Akalisahau mpaka gari lake!

# 6

*"Ukichagua kuwa mpelelezi, umechagua kuwa kisu cha jikoni. Leo utakata nyanya, kesho utamenyea maganda ya vitunguu. Lakini, ipo siku tu utapachikwa kwenye sehemu ya tunda iliyooza ili kuiondoa, na kule kuzima kunakobaki kuweze kulika...."*

Hii ni sura ya sita.

"Kijana! Oya! Kijana!" Inspekta alijitahidi kumuita yule mvulana aliyekuwa mbele yake akizichota hatua kwa uharaka.
"Umechelewa sana Inspekta. Hatuna muda tena!" Kijana alijibu.
Inspekta alimsikia kwani alishamkaribia kwa namna alivyokuwa akijitahidi kutembea ndani ya mwendo wa nusu kukimbia.
"Ni hivi, nimeacha gari langu kule nyuma, hatuwezi kulifuata tukaenda nalo?" Inspekta alisaili. Sasa

kumbukumbu zake zilifanikiwa kurejesha kichwani kile ambacho alikisahau.

Kijana hakujibu kitu.

"Eti, kwani huko makaburini ni wa..."

Kabla Inspekta hamaliza kuulizia umbali ama ukaribu wa huko lilipo kaburi...

"Tumefika!" Kijana alimjibu kwa kumkatiza.

Walikuwa mbele ya jengo kubwa la kifahari. Limezungushiwa ukuta.

"Ni humu? Kaburi lipo humu?" Inspekta aliuliza huku akipangusa jasho katika paji la uso kwa kidole na kulitupa chini.

"Hapana, ni nyuma ya hili jengo. Nyuma tu hapo!" Alijibu yule kijana na kuanzisha harakati nyingine za hatua zilizomlazimu Inspekta kumfuata.

Waliufuata ukingo wa ukuta mrefu uliokuwa umeizunguka nyuma hiyo mpaka walipofikia mwisho. Macho ya Inspekta yaliyokuwa yametingwa kulisaka hilo kaburi, yakakwaana na kibanda kidogo, kilichokuwa kimejengwa kwa mabati na kufunikwa kwa vitambaa vyeusi. Kijana alikuwa akikifuata kibanda hicho, Inspekta naye akageuka kivuli chake.

Walipofika karibu, kijana akamsogezea kipande cha tofali na kumpatia aketi.

"Nakuja!" Akatamka maneno hayo huku akifungua kile kitambaa cheusi na kupotelea kwa kuinama ndani ya kile kibanda.

"Ukichagua kuwa mpelelezi, umechagua kuwa kisu cha jikoni. Leo utakata nyanya, kesho utamenyea maganda ya vitunguu. Lakini, ipo siku tu utapachikwa kwenye sehemu ya tunda iliyooza ili kuiondoa, na kule kuzima kunakobaki kuweze kulika. Hatimaye leo upelelezi umenifikisha kwa mganga!" Alijizungumzisha Inspekta Kashmiri Kashmiri akipapachika umakini pale ambapo kijana yule alipotelea. Kisha akatoa simu yake kutazama saa na kugundua tayari ni saa nane na nusu. Kabla ya kuirejesha mfukoni, akapata wazo la kuweka sehemu ya kurekodi sauti ili chochote ambacho kingepatikana kwa kusikika mahala hapo kije kutumika baadaye kama ushahidi.

Mara, yule kijana akachomoka ndani ya kibanda, akifuatana na bibi aliyekuwa amemshika mkono. Wawili hawa walijongea mpaka pale alipokuwa

ameketi Inspekta Kashmiri Kashmiri. Inspekta akasimama kwa heshima na kusalimia.
"Shikamoo!"
Kwa kumtazama tu kikongwe huyo, moyo wa Inspekta ulikiri hatofautiani sana umri na mama yake aliyekuwa kijijini. Hivyo alistahili unyenyekevu wake. Kusimama kwake, ilikuwa ni kupisha yule kikongwe aketishwe pale ambapo alikuwa amekaa yeye.
"Marahabaa baba yangu!" Bibi aliitikia kwa uchangamfu baada ya kuwa yuko chini. Macho yake yalifunga muda wote. Alikuwa ni kipofu.
Hata vile vitenge vilivyokuwa vimeusitiri mwili wake, vilichoka kwa kuchakaa.
"Nikusaidie nini baba?" Bibi aliuliza. Sauti yake pia ilijaa unyonge na kutetemeka kwa kila silabi aliyoitamka.
Inspekta kabla ya kujibu, akamtupia jicho yule kijana akitegemea apate dira yoyote ya mazungumzo kutoka kwake. Tofauti na alivyokuwa akiwaza, kijana naye alitulia tuli kumsikiliza Inspekta akisema nini anachotaka kusaidiwa.

"Bibi, niko hapa kuulizia kaburi la Bibi... Bibi...." Inspekta alijaribu kukumbuka. "Kaburi la Bibi Mboga." Hatimaye jina likamrejea fikrani na akaweza kulitamka. Yule Kikongwe akiwa ndani ya uchangamfu, alimjibu, "Bibi mboga ndiye mimi, baba yangu. Na mule nilipotokea, nd'o kaburi langu!"

Inspekta macho yakamtoka! Akamtandika jicho la kwanini yule kijana, kijana hakuwa ndani ya mshangao wowote, akageuza mboni zake kule kilipo kile kibanda, hakuona kaburi!

'Kumbe sio mganga, huu upelelezi leo umenikutanisha na mizimu!'

Aliwaza huku akizishusha pumzi zake na kujipa ujasiri. Akaweka sawa miguu yake huku akiitikisa, na kuiuliza ikiwa iko tayari kwa kukimbia.

'Agh! Mbio? Tena za kukwepa kunyonywa damu? Hilo tuachie sisi!'

Yumkini miguu ilimjibu hivyo. Hata Inspekta akadiriki kutabasamu na kuhoji, "Kaburi? Kile si kibanda?"

"Kile kibanda unachokiona, ndiyo makazi yangu ya kudumu kwa miaka mitano sasa! Nashinda mule, nalala mule, lakini kwa kuwa maisha yangu yamekosa

maana kama mfu, kama maiti aliyezikwa, sina budi kuliita kaburi. Mimi ndiye Bibi Mboga. Na hilo ulionalo ndilo kaburi langu," alijibu yule bibi. Kauli iliyomfanya Inspekta Kashmiri kuweka sawa masikio na fahamu zake ili kuelewa kwa kina yale aliyokuwa akiyasikia.

Sasa haukuwa woga tena bali uliokuja kwa awamu ile ni udadisi. Inspekta Kashmiri Kashmiri akamsogelea yule bibi kwa karibu ili kuzungumza naye na kutaka kuijua mantiki ya kauli yake.

"Kwanini unajiita mfu hali ya kuwa unapumua bibi?" Inspekta Kashmiri alisaili, akiwa yuko wima vilevile.

"Baba yangu, hujanijibu swali lako, unanipa kazi ya kuyajibu unayouliza wewe. Hujasema nikusaidie nini?!" Bibi alitaka kujua kilichompeleka kwake.

Yule kijana aliyekuwa pembeni akaguna kidogo. Inspekta Kashmiri alipomtazama, kijana akampa ishara kwa mkono wake wa kulia kuwa anatakiwa ajieleze. Azungumze kile kilichomleta.

"Ah bibi," Inspekta akafungua bomba la kauli, "Nipo hapa kwa maelekezo ya Maya. Nimeelezwa nikutafute. Akanitajia na eneo."

"Maya?" Yule bibi alishangaa. "Maya ndiye nani?" Kisha akauliza.
Inspekta akatafuta jibu la haraka, "Yule binti mdogo. Yuko gerezani kwa sasa kwa kosa la mauaji. Amesema nikutafute ili nipate maelezo kwako. Mimi ni askari polisi."
"Anaitwa Maya?" Bibi akahoji.
Fahamu za Inspekta zikakwangua jambo, akapata la kuzungumza ili aeleweke zaidi, "Maya wa Ulaya!" Inspekta alilimalizia jina kama alivyowahi kutajiwa.
"Oooowh, binti yangu mkubwa! Maya wa Ulaya! Hapo sasa nimekufahamu!" Bibi aliitikia huku tabasamu likiwa limeenea mdomoni mwake.
Inspekta haelewi kile alichokuwa akikitazama.
Bibi akafunguka kitu kingine, "Maya wa Ulaya ni binti yangu. Ni msichana mkubwa sana. Na ameahidi kunifufua. Yupo anayapambania maisha yetu ili nirudi hai tena!" Kauli za kikongwe huyu zilijaa utata.
"Kwanini unasema umekufa bibi?" Inspekta aliuliza swali ambalo awali alipolitoa, lilikosa jibu.
"Yeah, miaka mitano nyuma, wapo watu wachache, wababe, waliokuja kupokonya maisha yetu ya furaha

na kututumbukiza katika kiza. Mimi na familia yangu. Tumeteseka sana! Sana! Wametutupa katika kifo. Hakuna mwanadamu wa kuthubutu kutuongelesha, kama maiti anavyosahaulika katika kaburi lake." Bibi bado alikuwa akizungumza mafumbo.

"Watu? Wakina nani hao? Na Maya ni mwanao? Unasema ni binti mkubwa, kwanini? Kwanini unamuita Maya wa Ulaya? Kuna nini nyuma ya hili?" Inspekta Kashmiri Kashmiri alitapika utitiri wa maswali. Shauku iliyokuwa ndani mwake kukifahamu kitendawili kile kigumu ilikuwa ni kubwa kuizidi subra.

Yule bibi alitabasamu, kisha akamjibu kwa ustaarabu kabisa, "Mbona umesimama baba yangu na maswali yako yanahitaji majibu marefu kiasi hicho? Hebu keti. Keti chini nikusimulie!"

Inspekta Kashmiri Kashmiri akaweka chini makalio yake, mchangani, bila kujali kuchafuka. Baada ya hapo ukafuata mkasa mzito uliokifungua kichwa cha askari huyu wa polisi. Akajikuta akigundua picha tofauti. Tofauti kabisa na ile aliyokuwa nayo tangu awali!

# 7

*"Katika ulimwengu wa sasa, mnyonge ananyongwa na haki yake wanaondoka nayo. Kidonda cha masikini kimekosa madeko kabisa! Pole atakayotamkiwa bila kutazamwa usoni huhesabiwa kama matibabu tosha kabisa ya kumpa ahueni. Na hakuna wa kutokea akajali!*

Hii, ni sura ya saba!

BIBI MBOGA ANASIMULIA...

"Maisha ya binadamu hayana tofauti na upepo wa ufukweni, ukipepea vizuri ni raha kwa wanaobarizi, na ikiwa kinyume chake huwa ni majanga. Hili halina utofauti na maisha tuliyokuwa tukiishi sisi. Hilo ghorofa unalolitazama, hilo jengo hapo, lenye ukuta, ndilo jengo tulilokuwa tukiishi. Mimi, mume wangu, pamoja na binti yetu, Maya.

Tulidumu katika furaha na amani. Mume wangu akiwa ni mfanyakazi wa kuajiriwa serikalini, kabla ya baadaye kuja kustaafu. Naye akawa ni mtu wa kushinda nyumbani. Pesa kidogo zilizokuwa zikipatikana kama mafao ya utumishi wake, zikatumika kuyasogeza matumbo yetu kwa njaa na shida za hapa na pale.

Ndani ya miaka miwili, pesa hizi zilikatika. Sijui zilibaki chache ama zilikwisha kabisa. Hili lilikuwa likijulikana na zaidi na yeye mume wangu. Lakini kwa hakika, wali wa kushiba huonekana kwenye sahani. Hali na muonekano wa mume wangu vilichoka. Mtoto wetu aliyekuwa masomoni bado alihitaji kupata pesa ya kila siku, achilia mbali yale mahitaji muhimu ya kitaaluma. Vyote hivi viliutegemea mfuko wa mume wangu uliokuwa umeanza kuweka alama za kuchanika...

Umaridadi huficha umasikini, na usafi wa koti hulisitiri shati chafu lililo ndani. Jambo la kushukuru, nyumba ya kifahari tuliyokuwa tukiishi, ikayaziba madhaifu na shida zetu. Tukabaki tunagugumia nazo ndani kwa ndani.

Hatimaye akapatikana mpiga ngoma aliyekuwa akilazimisha tuicheze. Kama kumbukumbu zangu ziko katika unyookaji, nadhani ilikuwa jioni ile, alitujia mgeni akiwa ndani ya suti kubwa na tabasamu pana.

Mavazi yake yalinifanya nimhisi ni rafiki wa mume wangu. Mavazi ya kiofisi. Lakini nilipokwenda kumuita na kumweleza kuna mgeni wake, naye pia alitoka kwa mtazamo wa kutokumfahamu. Alikuwa akimshangaa. Waliketi wakazungumza. Ndani ya dakika chache akaondoka na mume wangu kumsindikiza mpaka getini. Aliporudi, nilimsaili, nilimuuliza kuhusu yule mgeni, akanijibu ni mtu aliyetumwa kuja kuulizia ikiwa nyumba yetu ingeweza kuuzwa.

Na wewe umempa jibu gani?

Nakumbuka niliuliza hivyo. Mume wangu akatikisha kichwa kabisa kwa msisitizo na kumalizia kauli kuwa ni jambo lisilowezekana.

Huo ukawa ni mdundo wa kwanza. Na hakuna kati yetu aliyeuhisi wala kuuelewa. Tuliupotezea.

Ukaja mdundo wa pili ambao ulikuwa mkali zaidi. Huu ulitushtua. Baada ya wiki moja tukapokea ugeni mwingine wa watu watatu. Wawili kati ya hao,

hatukuwa tukiwafahamu. Yule aliyesalia ndiye ambaye alikuja siku ya awali akaelezwa nyumba haipo katika mipango yoyote ya kuuzwa. Kikao hiki cha pili sikutaka nikae mbali, nilishiriki. Nikayasikia yote. Wale watu walitoa karatasi ambayo ndani mwake kulikuwa kuna ramani kubwa. Sikuweza kuielewa, lakini nililiona neno Magomeni. Tukaoneshwa eneo la kiwanja cha nyumba yetu. Tulipokuwa katika bumbuwazi la kutaka kujua mantiki ya yote hayo, tukaarifiwa tumejenga ndani ya kiwanja kilicho kwenye mipango ya serikali. Na tunapaswa kuhama haraka kwani kuna kiwanda kikubwa sana kinachotakiwa kujengwa.

Unadhani tulipinga? Walaa! Mimi na mume wangu tulikuwa ni raia wema kabisa mbele ya mamlaka. Ila, tukahoji kuhusu fidia. Tuliulizia malipo. Pesa za kutuwezesha kupata makazi mengine. Na tulizungumza kiutaratibu tu. Hatukufoka.

Sijui ilikuwaje kauli zetu zikalakiwa na majibu katili namna ile! Mpaka leo nikitafakari sijui!

Unanisikiliza vizuri baba yangu? Hapa naizungumzia miaka mitano tu hapo iliyopita...

Basi, wale wageni wa mara ya pili wakaondoka. Nyuma wakaacha kauli ya angalizo na onyo. Tuhame ndani ya wiki mbili tu, kinyume na hivyo, maisha yetu yangekwenda kuhitimika gerezani kwa makosa ya kukiuka maagizo ya serikali.

Mume wangu, pamoja na umri kumtupa mkono, alijikongonya na kuanzisha safari katika ofisi za kimamlaka. Alianzia chini kabisa..

Mjumbe, mwenyekiti, mpaka kwa mkuu wa wilaya, kote huko aliulizia kuhusu mpango wa serikali na eneo letu tunaloishi, sentensi zao zikawa zimejaa alama za mishangao na viulizo. Walisema hawaufahamu mpango huo na hakuna kiwanda kikubwa cha kujengwa katikati ya makazi ya watu. Sheria haziruhusu. Mume wangu alirudi nyumbani akanieleza yote hayo, sura yake ilikumbatia furaha mno. Akitegemea yale mambo yangekwisha. Na hakuacha kukariri kwa kauli zake kuwa wale watu huenda ni matapeli.

Yakasinzia majira mafupi, yalipokuja kuzinduka, jua lilikuchwa na kiza kuingia. Tulipomaliza kupata chakula

cha usiku, tulilala. Haukuwa usingizi wa kheri. Usingizi ambao sitakuja kuusahau.

Nilishtushwa na hekaheka za mume wangu, alikuwa pembeni yangu, kitandani, alikuwa akitikisika. Mwanzo, nilihisi ni ndoto mbaya tu, nikasogeza mkono wangu kumtuliza huku bado nimeyafumba macho yangu.

Hazikuacha. Ikabidi niyafumbue ili niweze kumuamsha ikibidi. Ni hapo ndipo nilipogundua kitandani pale hatukuwa wawili. Bali wanne.

Mmoja kamshika usoni, mwingine ameketi tu pembeni.

Nilihisi ni mimi sasa ndiye nimeingia kwenye ndoto. Na ile methali ya usimwamshe aliyelala labda ndiyo imeanza kutenda kazi. Nilipoziweka sawa mboni zangu, ndipo nilipogundua lile nilitazamalo ni tukio halisi. Mume wangu alikuwa katika nukta ya mwisho kuupoteza uhai wake. Nikapiga kelele, kabla sauti haijafika hata katika vidole vya miguu yangu, nilidakwa na kubanwa. Kisha kitu chenye ncha kali sana kilianza kuchomwa katika macho yangu. Sijui ni bisibisi, sijui ni kisu. Sikuweza kuona. Walinitoboa kwa zamu. Jicho la

kulia kisha kushoto, la kushoto kisha kulia. Kwa idadi ya matundu waliyoamua wao. Na hicho ndicho kilikuwa chanzo cha huu ulemavu nilionao.

Hatukuwa na mtu mwingine wa kumpigia kelele ndani ya nyumba ile. Ni sisi na binti yetu mdogo aliyekuwa akisubiri kutimiza umri wa miaka kumi na moja.

Msichana wa kazi tuliyekuwa tukiishi naye kabla, tulishamuondosha katika kipindi kile ambacho pesa iligeuka ngumu, kama namna ya kubana matumizi.

Nilimkumbuka sana siku hiyo!

Nililia kwa kupiga kelele. Simu ilikuwepo, lakini haikuwa na maana tena katika mikono yangu. Macho yangu hayakuweza kuvuta taswira ya chochote zaidi ya kiza. Machozi yalivyonimwagika, bila shaka yalijichanganya na damu iliyokuwa ikinitiririka.

Maumivu, upotevu wa damu kwa wingi, vyote vikaungana kwa pamoja kuhakikisha fahamu zangu zinapotea.

Nilipozinduka, pembeni yangu alikuwepo shemeji, mdogo wa mume wangu. Alisimama kama msaada muhimu sana. Akalipia matibabu na hata kuhakikisha

zoezi la kumsitiri marehemu linakamilika kwa asilimia zote.

Wiki moja tu ya ujane na upofu, ilitosha wapiga ngoma kuja kuniletea mdundo wa tatu. Ni huu mdundo afande, ni huu mdundo ulioniachia funzo kubwa sana maishani. Katika ulimwengu wa sasa, mnyonge ananyongwa na haki yake wanaondoka nayo. Kidonda cha masikini kimekosa madeko kabisa! Pole atakayotamkiwa bila kutazamwa usoni huhesabiwa kama matibabu tosha kabisa ya kumpa ahueni. Na hakuna wa kutokea akajali!" Bibi aliweka kituo kifupi baada ya masimulizi marefu.

"Mdundo gani?" Inspekta Kashmiri Kashmiri aliuliza wa kihoro cha kutaka kujua...

Yule kikongwe akakohoa kidogo ili aendelee kusimulia!

# 8

*"Yapo maamuzi katika maisha, kuzaliwa kwake, ni kifo cha maamuzi mengine. Hata pale unapodiriki kuuosha mkaa kwa maji, lengo likiwa ni kutokuchafuka kwa vumbi lake utakapoushika, basi hakikisha unakijua mapema chanzo chako kingine cha moto..."*

Hii ni sura ya nane.

SIMULIZI YA BIBI MBOGA INAENDELEA...

"Huu ukawa ni mdundo wa mwisho. Na ulikuja kwa kunishtukiza sana. Kilikuwa ni kipindi muafaka kabisa cha mimi kuzoea ukurasa mpya wa maisha niliofunguliwa.
Walinipokonya uwezo wangu wa kuona, ila sio ubongo ulioshikilia kumbukumbu kamili. Ilikuwa ni jioni ile, siku ambayo Maya alinifuata na kunishika mkono,

akanivuta. Kama leo hivi nilivyokamatwa na kuletwa hapa.

Nilipomuuliza ni wapi anipelekapo. Akasema nje kuna wageni wapo na dada, wanatuita sote.

Unaweza ukashtuka utakaposikia kuhusu huyu dada. Yeye alikuwa ni mfanyakazi mwingine ambaye shemeji yangu alituletea. Atusaidie kutokana na hali yangu.

Sikuwa na wasiwasi. Nikahisi ni ujio mwema wa wale wanaonifahamu kuja kunisalimia. Kunijulia hali na kunipa pole.

Haikuwa vile ambavyo dhana zangu zilisimama. Wageni hawa walikuja na maneno yaliyokuwa yakitulazimu tuubadilishe uhalisia. Sisi wenyeji tuwe wageni, wao wageni wawe wenyeji. Walikuja na watu waliowaita ni polisi. Pamoja na mjumbe wa mtaa, huyu yeye alijitambulisha. Shinikizo la kuhama likiwa limevitawala vinywa vyao. Walihitaji tuondoke. Tena haraka sana. Na hatukuwa na muda. Tulitakiwa tuvitoe vitu vyetu nje kwa utaratibu ama waingie wao watusaidie kuvichomoa kwa kuvirusha.

Hatujajibu, tumeshapigwa vikumbo. Watu ambao walisema wao ni sehemu ya jeshi la polisi wakatuweka

kizuizini. Kila nilipojaribu kuufungua mdomo wangu kuhoji, niligongwa kwenye mwili wangu na kupewa tahadhari ya kuumizwa na tayari kule kupigwa tu yalikuwa ni maumivu tosha!

Maya wangu alikuwa ndani ya kilio kikali. Labda hakuwa katika umri sahihi wa kuelewa kile kilichokuwa kikiendelea, lakini, kelele zangu za kuomba wale washika mpini kutupa nafasi ya kujipapasa na kupunguza kuturarua kwa makali yaliyokuwa kwenye ngozi zetu, zilimtosha kutambua kuwa tumo ndani ya tabu. Hakuna aliyejali kati yao. Tulifukuzwa kama wezi na kutolewa nje.

Nilimuomba dada wa kazi achukue simu na ampigie mdogo wa marehemu mume wangu, ampe taarifa. Alifanya hivyo. Naye alikuja baada ya nusu saa, akatukuta tukiwa nje ya geti.

Aliingia ndani, akatoka zilipopita dakika kadhaa akigugumia na kuomba tuondoke haraka sana.

Tulikwenda kwake. Tukaishi hapo huku akituahidi kusimama mstari wa mbele kuhakikisha haki inatendeka na nyumba yetu kupatikana. Haikupita wiki. Mpaka leo hii unavyonisikiliza, hajulikani

anapopatikana. Alipotezwa na tusimfahamu huyo mpotezaji wa kumuuliza.

Akaacha familia yake isiyojiweza kwa ukamilifu wa milo mitatu. Hali yao haikuwa njema. Mbozi zangu hazikuwa wazi, lakini matundu ya masikio yangu yalikifu kuyasikia malalamiko ya mkewe.

Ndipo siku nilipochukua maamuzi ya kuondoka. Mimi pamoja na binti yangu. Ila, yapo maamuzi katika maisha, kuzaliwa kwake, ni kifo cha maamuzi mengine. Hata pale unapodiriki kuuosha mkaa kwa maji, lengo likiwa ni kutokuchafuka kwa vumbi lake utakapoushika, basi hakikisha unakijua mapema chanzo chako kingine cha moto. Mimi nikiri, sikuwa nikikijua chanzo changu kingine cha moto. Nilihama nilipokuwa nikiishi bila ya kujua ni wapi pengine pa kuishi.

Maya wangu, binti mdogo kabisa, akiwa mbele, mimi nyuma, tunaongozana, tuliukatiza mji wa Dar Es Salaam kwa kiza na mwanga. Hata tulipokwaana na jirani aliyekuwa akitufahamu. Ni mama wa watu mjane yule. Mumewe alishafariki kitambo kidogo.

Alituchukua na kutuahidi kutusaidia. Alipofika kwake, shauku ya kuusikia mkasa wetu ikampata. Huku swali muhimu zaidi kutoka kwake likiwa...

Pesa mlizouzia nyumba yenu zimekwenda wapi?

Alipousikia mkasa mzima unahusu neno kudhulumiwa na sio kununuliwa, akagwatuka kwa mshangao huku akiziponda simulizi za mjumbe wa mtaa huo. Simulizi zinazodai tunaishi maisha ya kifahari mno huko kando ya mji karibu na fukwe maarufu za bahari. Sikumbuki hata aliutaja ni ufukwe gani.

Ila, yule mama aliingiwa na ghadhabu za maamuzi, akaniahidi kwenda kufuatilia na ikibidi haki itendeke. Ahadi ya mwanzo ambayo haikutimia ikarejea ndani ya kinywa kingine. Kinywa hiki kingine hakikuchukua mwezi, kikapotelea huko ambako kile cha mwanzo kilikimbilia.

Sasa kama kilikimbia chenyewe, ama kilikimbizwa, mimi sijui. Lakini huo ukawa ndiyo mwisho wa mimi kumsikia. Na hata nilipowasaili wale wenye majaaliwa ya kuona, jibu likawa ni moja tu, amepotea!

Sasa fununu zikaanza taratibu. Fununu za ubaya wangu wa kutoa watu kafara. Zikapikwa habari

zilizopepea kwa wepesi mno, na kuwafikia wengi mtaani, kuwa, mimi hivi na upofu wangu, usiku ninaona, na huyu Maya wangu, ndiye mshirika mkuu. Kinapoingia kiza tu, tunazama ndani ya majukumu mengine ya kishirikina, ambayo yanahitaji damu za watu. Na yeyote yule wa kuthubutu, akashiriki kuzungumza nami, basi amekwenda na maji. Sijui ni nani hasa alikuwa ni msambazaji wa hayo.
Akili zangu zilijaribu kunigusia ni mjumbe, lakini imani zetu zimetufunza kuhusu kosa la kumdhania mtu ubaya.
Pale tulipokuwa tukiishi, ndugu wa aliyepotea wakaja kutufukuza na kuzomewa juu. Nilikuwa nikijikaza mno kutolia ili Maya wangu asilione chozi, kabla ya dakika chache kuja kushtuka, na kukuta tayari viganja vyake viko shavuni akinipangusa.
Kilikuwa ni kipindi kigumu sana ambacho nilitamani Mungu anipe wasaa wa kuzungumza naye ili nimuulize juu ya kile kilichokuwa kikivurugwa katika muundo wa maisha yangu.
Ni dhiki ileile inayoongelewa kufuatiwa na faraja ama ya kwangu ilikuwa ni nyingine?

Dalili za hiyo faraja hazikuwepo hata kwa harufu.
Ndani ya usiku huo, ambao tulifukuzwa, tulikutana na bibi ambaye, mara zote huuza mboga hapa mtaani. Huyu bibi tulimuungisha mno mboga zake, kila asubuhi aliyokuwa akipita nyumbani. Katika kile kipindi ambacho nyama hakuwa rafiki yetu wa kudumu ndani ya mlo. Ni huyu bibi ndiye aliyetuleta katika kibanda chake hiki. Akajitoa muhanga na kutusitiri.
Hakika aliye juu hana muda na aliye chini, siku zote hizo, sikujua kuwa nyuma ya nyumba yetu anaishi binadamu. Tena mwenye moyo mkubwa kiasi kile.
Hakujali maneno ya walimwengu, hakujali namna walivyopunguza manunuzi ya mboga zake, kwa kile walichodai anashirikiana na mchawi. Aliziba masikio. Akatenda wema ambao bila shaka utampeleka peponi. Kwani, asubuhi moja aliyoamka, na kwenda kwenye mihangaiko yake, hakurudi tena! Yeye hakupotea kama wenzake, aligongwa na gari. Akapata umauti palepale.
Kaburi lake lipo nyuma ya kibanda hicho. Mimi jina langu sio Bibi Mboga, sio. Hapa tulipo ndipo

panajulikana hivyo ukiamua kupaulizia. Kila mtu katika jamii hii ametutenga. Hakuna anayejua historia iliyojificha. Wote wameyashikilia mashairi ya wimbo mmoja. Na hawaelewi yanamaanisha nini. Nilijihesabu mfu na nikakosa imani ya kufufuka. Kama sio safari ya Maya wangu. Safari ya kwenda Ulaya. Akarudi binti mkubwa. Akarudi msichana mwenye maono na kutaka kuirejesha amani yetu. Leo hii tusingeongea kwa muda wote huu. Na ndiyo maana, sitaki aitwe vyovyote vile, zaidi ya Maya wa Ulaya!" Bibi akanyamaza kidogo.

Inspekta Kashmiri alikuwa amesimama, hakupata hata hamu ya kukaa, akili yake ilitekwa na maelezo ya bibi huyo yaliyokuwa yakifumbua fumbo kubwa taratibu.

"Maya alikweda Ulaya kufanya nini, na ni nani alimpeleka? Au alikwenda mwenyewe na kwanini unasema ameleta mwanga? Yani ameleta mwanga kwa kufanya mauaji kwa wasio na hatia?" Inspekta akatupa maswali mengi kwa pupa kama ilivyo kawaida yake.

"Kaniletee maji kijana wangu." Bibi alimsikiliza kisha akaomba yule kijana ambaye alikuwa pembeni akamletee kipoza koo.

Kijana huyo alivyokuwa akiinuka, Inspekta alimtupia jicho la kumfuatilia na kuhoji tena, "Huyo naye ni mtoto wako? Au ni nani?"
Bibi akacheka, kisha akamjibu kwa urefu na sauti yenye upole, "Baba yangu, taratibu, Maya wa Ulaya ni binti wa uhakika, na anaposema jambo anajua nini anamaanisha. Sio yule Maya aliyeondoka hapa nchini akilia hata akikanyaga chupa. Maya aliyekuelekeza kwangu ni binti ambaye hata ukimkita kisu cha kwenye koo, atacheka na kukusikitikia. Nina hakika hakuna wa kumzuia Maya katika mpango wake. Na ndiyo maana hata wewe leo umefika huku ikiwa ni sehemu ya mpango huo. Alishatueleza mapema. Hivyo usijali. Ujio wako ulijulikana hata kabla haujamfahamu Maya. Maya wa Ulaya!"

# 9

Alifika ndani ya gari lake na kuteremsha mshindo mzito wa pumzi. Alikuwa amechoka sana.

Nje ya vioo tayari giza la jioni lilikamata usukani kuusukuma ulimwengu. Alishukuru kutoka salama kwenye eneo ambalo aliingia tangu mchana wa siku hiyo. Akaitoa simu yake na kutazama kioo kilichokuwa kikiinadi kazi kubwa aliyokuwa ameifanya. Saa nne, dakika arobaini na sita, sekunde ishirini na mbili. Ulikuwa ni muda wa sauti aliyoichukua kwa kuirekodi kwa siri. Alihitaji kwenda kuitumia kuuendeleza upelelezi wake. Na kabla ya kutekenya funguo kuliwasha gari hilo, tumbo likamuwahi kuunguruma.

Njaa!

Hakuwa ametia chochote kinywani zaidi ya chai isiyo na vitafunwa. Kazi kubwa ambayo alipanga kuifanya ilimteka kiasi cha kusahau kuwa chakula ni hitaji muhimu la maisha ya binadamu miongoni mwa yale mahitaji makuu matatu. Akaondoka eneo lile

akidhamiria kupitia mahala wauzapo mlo wa haraka ili anunue. Ghafla, mvua ikatokea kusipotarajiwa na kuanza akiwa katikati ya barabara. Baridi likapuliza hata alipojaribu kuvipandisha vioo vya gari lake. Upepo mkali uliokuwa ukipepea ukamhakikishia kuwa vipimo vya urefu wake wala havikosekani katika maduka vya wauza majeneza...

Kwa kuujali uhai, akaliweka gari kando kusubiri hali ikae sawa.

Ni gari ndilo lilisimama, lakini macho yake yalikuwa ndani ya mwendo kukitalii kigiza kilichokuwa kimemzunguka. Taa chache za magari ya madereva waliokuwa wamemzidi ujasiri zilipita zikamwacha. Lakini, baada ya muda mfupi akawepo yule ambaye hakutaka kuukosa uungwana. Walau salamu tu.

Kilianza kioo. Agh! Hapana. Nimechanganya hapo. Ulioanza ni mlio. Akageuka kuutazama ule upande ambao sauti ya mlio huo ilikuwa ikitokea. Akagundua ni kioo chake cha upande wa kushoto kilikuwa kikigongwa.

Moyo ukamtetemeka. Akili yake ikayakumbuka maneno ya mwisho kabisa kupewa, punde tu, baada

ya kutoka kule kwa Bibi Mboga. Akataka kuwasha gari ili aondoke. Aliinusa harufu ya hatari. Kesi iliyokuwa katika mikono yake tayari alishairushia kitambaa cheupe na kukiri uzani wake ni mkubwa.

Kioo kiliendelea kugongwa. Mgongaji akachukua uelekeo mwingine wa maamuzi na kwenda kusimama mbele ya gari lile. Ni hapo ndipo Inspekta Kashmiri Kashmiri alipojikuta akiutazama mwili wa kiumbe wa kike unaoteseka ndani ya kipigo kikali cha matone ya mvua. Kipigo kisicho na mapumziko.

Haraka akakishusha kioo. Mwanamke huyo akafika mpaka pale, wakawa wenye kutazamana. Mmoja akisubiriwa azungumze shida yake.

"Samahani kaka. Nafika hapo mbele. Unaweza kunisogeza?" Sauti laini iliomba ihsani. Alikuwa ni msichana. Amevaa baibui jeusi na kujitanda. Macho yake yalijaa aibu na sura yake iliakisi kutokukipenda kile alichokuwa akikifanya. Hakuonekana kuwa na amani ya uombaji.

"Sawa," Kashmiri aliridhia na kuiondoa loki. Akamruhusu aingie.

"Sa'aalekum," Binti akatoa salamu baaada ya kuketi katika siti. Alivaa nguo pana, lakini kwa namna ilivyoingia maji, alivyoketi tu katika siti, ikazidi kunatana na ngozi yake. Mikunjo yote ya maungo yakaingia katika mnada wa bei rahisi.

Inspekta Kashmiri Kashmiri akaweka kando macho yake ya kiume baada ya kumuitikia. Zikawa dakika mbili za zimwi la ukimya, kabla ya kikohozi chepesi hakijatangulizwa na binti kujizungumzisha...

Yalianza maongezi kuzihusu mvua za Dar Es Salaam. Inspekta naye hakubaki nyuma, akazielezea vile zinaathiri kazi zao za kiusalama. Binti akashtuka baada ya kujua ni polisi. Kisha akatoa heshima ya saluti iliyomfanya Inspekta Kashmiri kuangua kicheko.

Wakatajiana majina. Khadija likawa ndilo jina la binti. Aliyejieleza kuishi Magomeni lakini alikuwa akielekea Mwenge kwenye shughuli ya harusi ifanyikayo usiku. Mvua ikapoa na Inspekta akawasha gari ili kusonga.

Safari yao ikawa ni ya mazungumzo mengi. Binti akiwa ndiye kinara. Tofauti na ule muonekano wa awali ambao Inspekta alimhukumu nao, alijawa na uchangamfu mwingi wa kauli. Mara zote Inspekta

alidumu akiitikia tu hata kwa yale ambaye hakuyasikia vizuri.
Ikafikia nukta ya wawili hawa kuagana. Kila mmoja aendelee na safari yake. Binti akashukuru kwa wema aliotendewa, Inspekta naye akajichekesha kwa kuigiza. Walau ile kero aliyoikaribisha sasa inakwenda. Kichwa chake kilijaa mambo mengi sana. Alihitaji mapumziko. Kumshusha Khadija garini kukampa nafasi ya kutafuta mahala apate chakula. Kisha huyo, ak'enda zake nyumbani. Akiamini asingekutana tena na kiumbe aitwaye Khadija!
Akiamini!

*******

Saa nane kasoro usiku. Usingizi wake ulikatishwa na mvua iliyokuwa ndani ya ushirikiano mzuri na radi kali. Alitambua ni majira hayo baada ya kutazama simu iliyokuwa kwenye chaji. Akaichomoa na kujiondoa kitandani. Alienda moja kwa moja katika meza ndogo iliyokuwa ndani humo. Alitumia mwanga wa nje

uliokuwa ukipenya kupitia dirishani, kabla ya kwenda kuwasha taa na kurudi. Akaketi kwenye kiti kilicho karibu na meza. Kisha alivuta mkoba wake na kulichomoa faili la kesi ya Maya. Akaliweka mezani na kulifungua.

Maelezo ya Maya hayakuwa yenye kujitosheleza kabisa ndani ya faili lile. Lakini yapo ambayo yalibeba ukamilifu. Na aliyategea ndoano nzuri iliyoyakamata yote kwa sauti ndani ya simu yake.

Akaifungua na kuianza kuisikiliza. Kisha akaweka mpaka pale ambapo, Bibi mzungumzaji aliomba aletewe maji. Alisikiliza huku akikamata kalamu yake na kunakili vitu muhimu ndani ya faili. Yalikuwa ni maelezo kumhusu Maya. Maelezo ya kutosha kabisa. Asingeweza kuimaliza yote, akawa mwenye kuirusha. Akijiahidi asubuhi ya kesho yake, kuwahi haraka ofisini kwenda kuendeleza mahojiano na muhusika mwenyewe. Maya. Ikibidi akakanushe ama athibitishe.

Ghafla, simu ikakata ile sauti na kuanza kuita. Namba ngeni. Hakuwa ameihifadhi simuni mwake. Aliitazama kwa umakini sana kabla ya kuipokea.

"Inspekta, huwezi amini, hii mvua bado tu inapiga!" Sauti laini ya kike ililalamika.

Inspekta Kashmiri Kashmiri akabaki kimya. Akili yake ilikuwa ikiamini sauti ile ameisikia mahala.

"Sa'alekum Inspekta. Mie Khadija!" Mpigaji akajitambulisha. Alikuwa ni yule binti ambaye alimpa lifti jioni ya siku hiyo.

"Khadija?!" Inspekta akalirudia jina kwa mshtuko. Hakuwa amempa namba binti huyo. Kaipataje?

Khadija aliitikia, "Ni mimi Inspekta. Nipo nje ya geti lako. Naomba unifungulie tuongee kitu. Ni muhimu sana kwa uhai wako."

"Nje ya geti langu? Tuongee? Umepajuaje kwangu?" Inspekta sasa alianza kufoka kwa kuuliza.

"Inspekta. We sikiliza..." Yule binti aliomba Inspekta Kashmiri agete sikio.

Mara, 'Ngo! Ngo! Ngo!'

Ni kweli. Geti lilikuwa likigongwa!

# 10

Unakutana na mtu, humjui. Unampa msaada. Baadaye mnaachana. Unafika kwako, usiku, usiku wa manane, simu yako inaita. Unapoipokea, mpigaji anajitambulisha ni yule mtu uliyempa msaada. Hiki ndicho kigugumizi kilichokuwa kikimtanza Inspekta Kashmiri Kashmiri alipokuwa akiusikia mlio wa geti lake likigongwa.

"Inspekta. Umepokea tu simu nikakueleza kuhusu mvua huku nje. Nalowa mwenzako. Uje unifungulie," Binti aliyejitambulisha kwa jina la Khadija alilalamika, sauti yake ilijaa upole.

Bado simu ilikuwa mkononi mwa Inspekta. Alikuwa na hofu. Alianza kuvuta picha, yumkini huyo mzungumzaji simuni tayari yumo ndani. Kama ameweza kumpigia bila ya kumpa namba yake, angeshindwaje kuingia bila ya kufunguliwa?

"Inspekta. Nipo hapa kukusaidia. Si kwa shida yangu. Nipo hapa kwa ajili yako!" Khadija aliendelea kusisitiza.

"Sifungui. Ondoka!" Inspekta alijikaza na kufoka.
"Nikiondoka, hutaelewa chochote kuhusu Maya!" Khadija alizungumza na kulitaja jina lililovuta akili ya Inspekta Kashmiri.
'Anamfahamu Maya?!'
Inspekta alijihoji huku akiitoa simu sikioni na kuitazama namba kwa mara nyingine.
"Okay. Kwa kuwa umeamua kutokunifungulia. Sawa. Nitaongea nikiwa hapa hapa nje," Khadija akakubaliana na yote. Kisha akafunguka jambo, "Najua umeelezwa kuhusu safari ya Maya. Unajua ni nani aliyempeleka?"
Inspekta akajibu kwa dharau,"Sina shida ya kufahamu. Ninachotaka unieleze huyo aliyekupa namba yangu."
Khadija akacheka simuni. Naye akatoa kauli iliyokuwa imebeba chembe ya kejeli, "Mie nikajuaga hilo jambo wanaulizaga mabinti. Kumbe hataa weye?" Akamalizia kwa swali. Lafudhi ya msichana huyu ilikuwa ndani ya asili ya upwani.
"Sitakuja kukufungulia mpaka utakaponieleza umeipata vipi namba yangu!" Sasa Inspekta Kashmiri naye akatuma mtego wa tamanio. Kwamba,

angejibiwa swali lake, basi angekwenda kufuungua. Bado mvua nje iliendelea kupiga kwa fujo.
"Inspekta. Nafahamu umeshatambua Maya ni binti aliyekuwa ameingizwa katika mpango mkubwa sana nchini Italia. Mpango wa kutengeneza mabinti hatari zaidi katika ulingo wa mapigano ya kuua. Lakini, kuanzia leo, elewa kuwa, mimi nilikuwa miongoni mwa wasimamizi wa mradi ule, mradi bado haujakufa. Nipo hapa kumchukua Maya. Na hakuna mwingine wa kunikutanisha na binti huyo zaidi yako Inspekta. Kesi hii imo mikononi mwako. Sijali chochote kuhusu wewe. Ukiwemo uhai wako. Leo umegoma kunifungulia mimi kuingia ndani. Itafika zamu yangu ya kugoma kukufungulia kutoka nje! Mwambie Maya El Madame namsalimia. Kumbuka, ni El Madame!!!" Khadija baada ya kuushusha mzigo wa maelezo na mkwara, akakata simu.
Inspekta Kashmiri akaitazama simu yake na kuiweka katika meza.
"El Madame!! Mbona mnataka kunivuruga sana sasa?" Kisha akaizungumzisha kama vile ilikuwa ikimsikia.

Akaikamata tena, haraka akaipiga ile namba, haikupatikana. Swali la namba yake imepatikana vipi halikutolewa jibu. Akaliacha tena lile faili na kuigemea meza yake kwa majuto. Maamuzi yake ya  kutaka kuingia kwa mara nyingine katika kesi hiyo shauri ya kisasi, yalianza kumgharimu.

Kule kwa Bibi Mboga, bibi aliyegoma kabisa kujitambulisha kwa jina lale, alielezwa kuwa Maya alikuja kuchukuliwa na watu waliojiita ni watu wa kanisa. Watu hawa wakamchukua na kuahidi kwenda kumpeleka masomoni. Nje ya nchi. Huko, likatendeka lingine kabisa. Wala hayakuwa masomo ya kawaida. Yalikuwa ni masomo ya ujasusi. Mabinti wadogo walikuwa wakifundishwa kuwa watu wazima kififikra. Walifundishwa namna ya kumshambulia mtu, kwa kasi, mithili ya chui awindaye swala aliye mita moja mbele yake, wakaelekezwa namna mifumo mbalimvali ya kiusalama inafanya kazi. Mifumo ya nchi zote duniani. Kisha wakapewa muda wa kusoma sana vitabu. Vitabu vya mafunzo ya kipelelezi na ujasusi, riwaya za kipelelezi, vitabu vya kisaikolojia na vitu vingi kuuhusu ulimwengu. Yote hayo Maya alimuhadithia mama yake.

Na ndiye aliyekwenda kumsimulia Inspekta Kashmiri. Mwanaume ambaye kichwa chake kilianza kuingia katika tafsiri halisi ya wendawazimu. Hata kabla hajapata ufumbuzi kuhusu mkasa huo wa Maya na namna ulivyokuwa ukiunganika na kesi iliyopo mbele yake, likaja lile la Khadija lililomfanya achoke na kulegea mwili wote.

Akiwa pale katika meza, ndani ya mawazo yenye vitendawili vingi, usingizi ambao awali ulimponyoka bila sababu ya uhakika, ukamrejea tena bila sababu ya kueleweka.

Hapakuchi pakakucha. Sauti za kuwika kwa majogoo ndizo zilizokuja kumzindua. Alipotazama saa yake, aligundua tayari sekunde zilikuwa kwenye msongamano mkubwa sana kuiunda saa mbili kasoro. Hakunywa chai. Akajitundika sare zake za kazi na kuelekea ofisini. Huko, hakwenda kokote kule zaidi ya kumtafuta mkubwa wake. Akamkosa. Hakuwa amefika. Jambo ambalo alilihitaji lilitaka ukamilifu wa mapema. Akampigia na kuwasilisha ombi. Ombi likakubaliwa. Baada ya nusu saa, ama zaidi, Inspekta akawa ndani ya

chumba cha mahojiano, mbele yake akiwepo msichana Maya. Wanatazamana.
"Sura yako inaonesha kufahamu mengi sana kuhusu mimi Inspekta. Tofauti na awali!" Maya alizungumza, akakaa kimya kidogo na kuendelea, "Paji lako la uso limeshuka, mashavu yako yamekaza kuashiria kujiamini. Inspekta, hongera kwa kuitimiza kazi niliyokutuma. Sikutegemea ungeifanya mapema hivi!"
"Unaweza kunieleza, hawa waliokupeleka Ulaya, nchini Italia, walikuwa na lengo gani kwako?" Inspekta akahoji kutokana na maelezo aliyokuwa ameyapata.
Maya akatabasamu kidogo, alifurahi, alifurahia kitendo cha Inspekta kuyapata maelezo kumhusu. "Nilienda kufanywa kuwa muuaji," akajibu.
"Kwa hiyo umekuja nchini ili uue?"
"Ndiyo Inspekta. Nimekuja kuua Inspekta," Maya hakuwa na hata nukta ya woga wala mashaka.
"Vizuri. Unaua ili ulipe kisasi. Ndivyo?" Inspekta akapenyeza swali ili aujaze upelelezi wake. Lengo, atumie kauli ya Maya, kama ushahidi, na kuifunga kesi hiyo, ikibidi, ikasogezwe katika mamlaka za juu zaidi za kijeshi. Haikuwa kesi ndogo. Haikuwa kesi ya kawaida.

Haikuwa kesi ya mchezo mchezo. Ilishamvuruga. Ilishavamiwa na madoa ya kijasusi na mambo mzito. Huo ulikuwa ni mzigo mzito kwa Inspekta. Yeye alishasamehe kuhusu Gwaya. Aliamua yaishe. Na maisha yake yaendelee.

Lakini, haya, yakawa ni maji ambayo aliyavulia nguo. Kuyakoga ni wajibu ambao ulisimama mbele yake ukimtazama kwa huruma.

"Inspekta. Nikueleze mara ngapi?" Maya akajibu kwa swali lile jambo la kuua ama kutokuua alilosailiwa.

"Hivyo unalipa kisasi cha familia yako?" Inspekta akanogewa. Swali la ziada likamtoka.

"Ndiyo. Na bado watu watatu katika orodha yangu. Wawili utawaweza. Wa mwisho utakuja kunitoa ili nikusaidie!" Maya akajibu huku akiwa ndani ya tabasamu lake lililozoeleka.

"Unamfahamu El Madame?" Inspekta akaingiza swali ambalo, laiti angejua, laiti, laiti....

Asingelitamka hata kwa herufi moja!

Maya alishtuka kwa kulirudia jina, "El Madame!!!"

Inspekta akajibu huku akitabasamu kwa kuuona wasiwasi wa Maya kwa mara ya kwanza tangu aanze kukutana na binti huyo. Akaamini amemuweza.

Maya alikuwa amefungwa. Mikono na miguu. Kwa minyororo. Akajikunja. Kwa namna ya ajabu sana. Akakifikia kichwa chake na kujipapasa. Alitoa kitu mithili ya chuma kwenye nywele zake. Kitu kidogo mno. Kama kipini, kama kifunguo. Hakikueleweka. Hakukiona vizuri Inspekta shauri ya kushangaa binti huyo alivyokuwa amejikunja kama mpira, kama asiye na mifupa, kama amevunjika vunjika. Kisha, akaanza kuzifungua pingu zake kupitia kifaa hicho.

Mpaka Inspekta alipokuja kuzinduka kwa fikra, ilibaki miguu pekee kuwekwa huru.

Ndipo Maya alipokifungua kinywa chake na kuzungumza, tena kwa dhati takatifu kabisa, "Nilitegemea hili lingekawia kuja Inspekta. Lakini imekuwa haraka mno. Naomba asitokee wa kuthubutu kunizuia. Kama nilivyoamua mnikamate. Na sasa nimeamua nitoke. Asithubutu wa kunizuia Inspekta. Sijisikii kumwaga damu za msio na hatia!"

# 11

*'...Kuhusu maisha, kwamba, ni zawadi ya mara moja isiyojirudia. Unapojikuta umo ndani ya zawadi hiyo, hakikisha unaitumia vizuri kabla ya yule aliyekukabidhi kuichukua. Ni hapo ndipo alipoambiwa kuwa dunia haitaki viumbe wanyonge. Inahitaji watu jasiri na wenye roho ngumu. Kinyume na hivyo angejikuta ni kiumbe dhaifu anayeshindwa kuendana na changamoto za walimwengu...'*

Labda kwa imani, labda kwa mikasa ya waliofeli waliowahi kubadilika na kuingia katika kundi la wenye mafanikio, pengine ni miongoni mwa vitu vilivyomsaidia na kumeza kauli ya hakuna kinachoshindikana katika dunia. Mwanamke ambaye alikuwa akihitaji kupata mtoto tangu katika umri wa miaka ishirini, akaja kumpokea kwenye arobaini iliyokuwa ikizipiga hatua kali sana kuiwahi hamsini. Ingetosha kumuita mzee. Lakini kwa yule mtoto

ambaye alizaliwa, alikuwa ni mama kama mama wa wengine. Mama aliyekwenda kuingia katika matatizo makubwa yaliyopelekea kupoteza hata uwezo wake wa kuona.

Mungu hakupi kilema akakunyima na mwendo. Huyu mtoto wa uzeeni akasimama kama msaada mkubwa mno kwenye kumuongoza njia pale ilipobidi. Wakahangaika huko na huko. Mwishowe walikata tamaa. Kwenye vipindi vyote hivyo vya mateso yaliyosabanishwa na binadamu, mzazi akiamini mtoto wake mdogo haelewi chochote, binti aliendelea kuuchora mchezo mzima huku akimshitakia Maulana akiamini hayupo mwingine wa kuingilia kati. Baba alishafariki. Na kila aliyethubutu kuwasaidia kwa lolote, angepotezwa kwenye uso wa Dunia.

Ni wa kina nani hao?

Bunti hakuwajua. Lakini, ilikuwepo sura moja, sura moja, ambayo ililala vema katika kitanda cha kumbukumbu zake. Akihakikisha iko salama muda wote, ili siku ambayo angeizindua, basi aketi na kuzungumza nayo, impe majibu sahihi.

Na huo wakati wala hakuwa kwenye masafa marefu. Kibanda chao walichokuwa wakijisitiri, kikapokea ugeni ndani ya jioni moja. Ugeni wa ghafla. Kundi la watu lenye vitabu vitakatifu mikononi, na yale mavazi yao yaliyokuwa yakithibitisha ni nyoyo zilizoshiba maadili.

Huku tabasamu likiwa limepamba vinywa vyao karibu vyote, walizungumza kuhusu ufadhili wa kimasomo. Wakimhitaji yule binti mdogo ili wakamuendeleze. Ahadi zao zilipendeza. Ilikuwa ni miti yenye matunda mbivu katika kila tawi. Mama hakuweza kujizuia. Huku machozi yakimtoka kwa kufahamu faraja pekee iliyokuwa karibu yake, hata kama hakuwa akiweza kuitazama, ilikuwa ikienda mbali ambapo asingeweza kuihisi hata kwa sauti.

Haikuwa rahisi kwa binti pia. Alilia kuiacha amani yake na kukubali kuelekea asipopajua, kwa watu asiofahamiana nao, ili kuzitimiza ndoto zake za kuwa rubani.

Na hili ni swali ambalo aliulizwa alipokuwa ndani ya ndege kupelekwa nje ya chini.

"Maya, unataka kuwa nani?"

Alipojibu rubani, wale waliokuwa wakilisubiri jibu wakaangua kicheko kikali kwa kuhisi binti alibeba uamuzi huo kwa kuwa alikuwa ndani ya ndege. Na wakaleta mzaha, kwamba, labda angekuwa ndani ya boti, si ajabu binti huyo angechagua kuwa nahodha. Nyuso zikaingia tena katika vicheko vizito. Binti akaamini yupo na watu wazuri. Zile bashasha alizoamini zingedumu, zikabadilika punde tu baada ya ndege kutua kwenye ardhi. Nchini Italia. Kwenye uwanja wa kimataifa wa Leonardo da Vinci, 'Leonardo da Vinci—Fiumicino Airport', uliopo katika jiji la Roma. Hapo akaongozana na msichana aliyelekezwa amuite kwa jina moja tu, ambalo alisisitiziwa kuliweka kichwani, El Madame!

Safari yao ikaukamata ukomo katika jiji la Genoa. Wakitumia takribani masaa matano kwa treni. Wakachukua taksi, mwendo wa dakika ishirini wakaufikia ukomo.

Waliingia katika kanisa. Ndani ya kanisa hilo, wakaelekea moja kwa moja kwenye chumba. Baada tu ya kuitumbukiza miguu yao minne ndani kwenye chumba hicho, sakafu ikateremka mpaka chini, mithili

ya lifti, na kuingia kwenye ulimwengu mpya kabisa ambao binti Maya alitambulishwa. Akapewa kanuni kadhaa za mwanzo kama ufunguzi.

Alitakiwa atambue kuwa kama alivyokuja hapa duniani peke yake, basi aishi hivyohivyo. Asimuamini mtu. Asiweke mategemeo kwa yeyote. Akaelezwa kitu kuhusu maisha, kwamba ni zawadi ya mara moja isiyojirudia. Unapojikuta umo ndani ya zawadi hiyo, hakikisha unaitumia vizuri kabla ya yule aliyekukabidhi kuichukua. Ni hapo ndipo alipoambiwa kuwa dunia haitaki viumbe wanyonge. Inahitaji watu jasiri na wenye roho ngumu. Kinyume na hivyo angejikuta ni kiumbe dhaifu anayeshindwa kuendana na changamoto za walimwengu. Maneno haya ndiyo yaliyofungua nafasi ya kupokea darasa la ukakamavu. Maya alikutanishwa na mabinti wengine waliokuwa na umri wenye kushabihiana na wake. Akaelezwa majina pekee ya kuitana ni 'sisters'. Hakuna kujuana kwa majina yao halisi. Na yeyote ambaye angethubutu kulitaja jina lake, hilo lingekuwa kosa namba moja lenye kumwezesha kukata tiketi kwa safari yake ya kiroho kisha mwili wake akaucha duniani ili ufukiwe,

kama sio kuuchomwa. Waliambiwa asingetokea mtu wa kumfanyia mazishi ya kistarabu yule aliyekufa kwa sababu ya kuukosa ustaarabu. Dawa ya moto haijawahi kuwa maji.

Kisha, kila binti mmoja kati ya hao, alikuwa na msimamizi wake binafsi kutokea huko ambako alichukuliwa. Na msimamizi huyo, ni yule ambaye aliambiwa amuite 'El Madame!'.

Maya naye akawa na "El Madame" wake. Huyu 'El Madame' anakuwa na mafunzo kamili, kama yale ambayo walipaswa kupatiwa hawa mabinti, kasoro tu, umri wao ni mkubwa. Kinyume na malengo ya programu hiyo, inayohitaji mabinti wadogo.

Maya akajikuta ameingia ndani ya picha nyingine ya maisha. Aliingiza kwenye tumbo lake kile alichotakiwa kula, akakiweka katika matendo kile alichoelezwa kukifanya. Hakuwa na uhuru binafsi. Ndani ya umri mdogo akajikuta akifahamu mambo mengi kuhusu ulimwengu. Alizifahamu dini nyingi bila ya kukanyaga kwenye nyumba ya ibada. Akawajua madaktari na taratibu zao na hajawahi kuingia wodini. Ilitumika miaka miwili kuwatengeneza binadamu wenye uwezo

mkubwa kuuzidi ule unaoweza kufikiriwa. Ubongo wa Maya ulipokomaa, ukajikuta umeiamsha rasmi ile picha ya sura aliyoilaza. Binti akaitafuta nafasi. Ulipopatikana upenyo tu, akatoroka kambini na kukimbilia Tanzania. Akaweka ramani na mipango sawa. Sehemu ya mpango huo, ni kukamatwa na polisi. Kujikamatisha baada ya kufanya matukio kadhaa ya mauaji ya wale alioamini wameidhulumu familia yake. Akamuahidi mama yake kumrejesha katika nyuma yao. Mama naye akaahidi asingekwenda kokote mpaka siku atakayorudi kwenye nyuma yao. Akiwa ndani ya mchakato huo, taarifa inamfikia kutoka kwenye kinywa cha Inspekta. Taarifa kumhusu El Madame!

Kwamba anasalimiwa naye. Haikuwa salamu ya kawaida. Na Maya anawajua viumbe wa namna yake. Ile ilikuwa ni habari... Kwamba...

'Tayari nimeshapafahamu ulipo. Muda wowote, nikiamua kukujia, basi nakufikia!'.

Ndiyo sababu iliyomwaminisha Maya kuwa hana muda tena. Akautumia udhaifu wa polisi kumkata mtuhumiwa na kuacha kumpunguza nywele. Ama kuzitoa zote. Labda walikuwa wakizingatia haki za

mtuhumiwa. Labda hawakujua uzito wa mtuhumiwa aliye mikononi mwao.

Labda...labda....labda...

Hizi 'labda' zingetosha kabisa kuwasogeza mbali na lawama, ikibidi kuwaacha salama, wasidhurike kwa chochote ama lolote.

Kilichowaponza, ni kujaribu kumzuia Maya asitoroke. Waliamua, kwa utashi wao, kuyasimamisha mafuriko ya maji kwa mkono!

# 12

*'...Nyoyo za wasichana hawa zilikuwa zimekufa. Walipofundishwa namna ya kuzitoa roho za binadamu wenzao, walifurahia. Muhimu vile ambavyo walidumu kutokuvipata, walivipokea walipovihitaji. Walifunzwa kila kitu kuhusu ulimwengu.*
*Kisha, wakavishwa taji la utukufu. Walihakikishiwa kuwa wameshatoka kwenye utumwa waliokuwemo, na sasa ni zamu yao kuwatumikisha wengine.. '*

CHOCHOTE kinachojiri ndani ya chumba maalum cha mahojiano, 'interrogation room', huwa kinarekodiwa. Wala hakuwa Inspekta wa kulaumiwa, ni wale waliokuwa wakifuatilia mazungumzo yake na Maya. Ni wao ndio walioitisha kengele ya hatari, askari wenye silaha wakawa wamekizunguka chumba kulia na kushoto. Vishindo vya hatua zao vilisikika na Maya.

Ambaye, muda huo tayari alishavifungua viungo vyake vyote kuingia kwenye uhuru kamili. Binti alijichota mithili ya mshale na kutua nyuma ya Inspekta, alikwenda kumnatia mgongoni. Akamkwida kwa roba kali akiichomoa bunduki iliyokuwa kwenye kiuno cha askari huyo na kumwekea kichwani kwake.

"Inspekta. Sina mpango wa kukudhuru. Ninahitaji ushirikiano wako!" Maya akaikaza ile sauti yake ya kike huku akikoroma.

Inspekta Kashmiri bado alikuwa haelewi atetende nini. Kile kilichokuwa kimetawala fikra zake ni kuhisi binti huyo alikuwa akihitaji kumtumia kama mateka. Kwamba atoke naye akiwa amemwekea silaha kichwani na kuwashurutisha asifuatwe ama kufanywa chochote.

Hakuwa sahihi.

Hiyo ni mbinu ya wapambanaji wenye woga, lakini sio Maya. Yeye hakumhitaji Inspekta, badala yake akamshuruti aondoke ndani ya chumba kile na kumuacha peke yake. Maya alitaka abaki mwenyewe. Alitamani hilo ili hao waliokuwa wakija kumshika, awaoneshe namna gani mtu huwekwa kizuizini.

Inspekta Kashmiri tayari alishauonja moto wa binti huyo, na hakutaka kuupata kwa mara nyingine. Alitoka kama alivyotakiwa. Maya akabaki mwenyewe katika chumba. Na kwa sababu ambazo binti huyu aliamini ni za muhimu, alizirukia haraka sana kamera mbili zilizokuwa ndani ya chumba hicho na kuzivunja.

Inspekta Kashmiri alivyotoka akiwa mpweke, wale askari wengi waliokuwa nje, wakamfuata na kumkagua, walipojiridhisha yuko sawa, wakazivuta hatua zao na kuviingiza ndani viwiliwili vyao ambavyo walivikosea huruma.

'Maya leo hana minyororo jamani, msiingie nyie!'

Labda tungelipa kinywa jicho la Inspekta, lingetamka maneno hayo,  kwa namna alivyokuwa akiwatazama pindi akiwekwa kando ili watu wafanye kazi yao. Ama walau angewashauri wakaongeze idadi tofauti na ile ya watu watano waliokuwa nayo.

Mguu funika, mguu funua... Askari wa kwanza kutanguliza wajihi wake ndani, akarushiwa teke kali sana la kwenye kona ya taya, hapohapo, kishindo kikubwa kikathibitisha kuwa mwili umeshakutana na sakafu.

Wanne waliokuwa nyuma wakashtuka. Labda ni kwa hasira, ama kwa kusahau, kuwa, zao la hiyo hasira siku zote limedumu kuwa ni hasara...
Na haikuwepo hasara nyingine kwao zaidi ya maumivu ya viwiliwili vyao! Hakuna hata mmoja kati yao aliyefanikiwa kurusha walau risasi moja kutoka kwenye bunduki walizokuwa wamezikamata. Jambo la kusikitika zaidi ni kitendo cha Maya kutuzimia zile kamera mbili zilizokuwa ndani ya kile chumba, yumkini dunia wakati huu ingekuwa imepokea kumbukumbu bora zaidi ya video ya mapigano tangu iwahi kuumbwa. Ngumi zilirushwa na kutua kwenye maeneo muhimu. Haya maeneo hujulikana na watu waliojifunza mashambulizi ya kibaiolojia tu, kama Maya. Lilitafutwa koo likatekenywa, ikasakwa mbavu laini isiyokomaa kiasili na kupapaswa, iliwekwa sawa chembe ya kifua na kukitwa... Ndani ya dakika moja na nusu wanaume wote watano wakawa chini wakiugulia maumivu ya nusu kifo ama nukta chache kuuelekea umauti.
Maya akatoka nje ya chumba na kuanza kutazama kushoto, kulikuwa shwari. Na kile alichokifanya,ndiyo kanuni ya watu wa kiintelejinsia ilivyo. Wao huanza

jambo lolote upande huo, kisha huja kulia. Kinyume na watu wa kawaida. Nd'o maana katika amri zao za mwendo, utasikia, "kushoto,kulia! Kushoto, kulia!", na sio, "kulia, kushoto! Kulia, kushoto!". Maya alipoubadilishia uso wake upande wa kulia, kwa mbali, aliona mwanaume akiwa ameongozana na mwanamke, wakitokomea kwenye kona ya mwisho wa korido hiyo...

Yule mwanaume alishamtambua, ni Inspekta Kashmiri Kashmiri, mwanamke bado, lakini, pua ya binti huyu ilikuwa katika kumbukumbu sahihi kabisa na harufu ilioipokea..

Harufu ya manukato, manukato ya El-Madame!!!

"Shit! Anampeleka wapi Inspekta huyu Ibilisi?" Maya aling'aka akiziwahisha hatua zake kuwafuatilia!

*******

Mwenyeji wa Tanga. Kama vipo vitu ambavyo alibaki kuvijutia maishani mwake, ni siku aliyochukua uamuzi

wa kutafuta kazi katika nchi za Kiarabu. Karibu miaka kumi iliyokuwa imepita.

Alipata nafasi nchini Dubai. Baada ya taratibu za kughushi vyeti na kutoa sababu zisizo za kweli, safari yake ikabeba hatua ya kwanza.

Alikwenda katika nyumba, kama ambavyo alielezwa. Lakini, kitu ambacho kilikuja kujenga utofauti kwenye safari hiyo na kuweka alama ya hatua ya pili, ni majukumu ambayo yaliangushwa na kinywa cha mwenyeji wake. Mwenyeji huyu aliyetaka kuitwa kwa jina la 'Madame', aliwaingiza katika dimbwi la mabadilishano ya utu na fedha. Alitakiwa kujiuza. Alilazimishwa kuwa changudoa.

Hakuwa na ujanja wowote, kwani, mara tu alipofika nchini humo, alipokonywa pasi yake ya kusafiria. Akiahidiwa kurejeshiwa baada ya kipindi cha miezi mitatu ya kutenda kazi aliyotamkiwa. Kazi ya kuyatanua mapaja na kupokea kipande cha nyama cha binadamu mwenye matamanio yake. Alianza, akaifanya, mwanzo ulikuwa mgumu ila baadaye akazoea. Zipo siku ambazo alilifurahia tendo, na zipo siku 'mibaba' ilitoa miguno juu ya kifua chake na uso

ameukunja. Kukubali au kukataa kulikuwa kwenye hatima ya kufanikisha kuipata pasi yake ya kusafiria.

Alikuwa ndani ya kiza hicho cha utumwa hata ulipokatiza mbele yake wakati aliokutana na malaika ambaye alikuja kwenye umbile la kishetani. Mwanaume wa kiitaliano aliyekuwa fundi wa kuzungumza lugha nyingi. Mwanaume huyu walivyoingia faraghani, badala ya kufungua zipu yake ya suruali, akaifungua ile ya pochi na kutoa pesa. Akamkabidhi. Kidogo akatae, kwani ilikuwa ni kinyume na utaratibu. Mtu pekee aliyekuwa akipaswa kupokea pesa, ni 'Madame'. Na wa kuthubutu kukiuka hilo, adhabu ndogo kati ya nyingi ni kunyimwa chakula kwa siku nzima, kisha kuchomwa kwa pasi yenye moto mkali kwenye maungo ya mwili wako.

Yule Muitaliano alisisitiza sana. Akidai kuwa yuko pale kumsaidia. Binti naye aligoma, hakuwa akimuamini. Na hata angemwamini, hakuwa tayari kupokea maumivu ya kuungua ngozi yake, yale ya kwenye via vya uzazi, shauri ya wageni wenye 'vimo' tofauti—yalimtosha.

Muitaliano huyu akawa hakauki kuonana naye. Alifululiza siku tano. Zote hizo hafanyi chochote. Ni ushawishi tu. Alikuwa akimshawishi kumtorosha. Kuondoka naye nchini humo na kwenda naye Ulaya.

Zilivyokatika wiki mbili za marudio ya maneno ya namna moja kwenye mifereji ya masikio yake, binti akaridhia. Alikubali.

Hii ikawa hatua ya tatu ya safari yake!

Ndege moja kwa moja nchini Italia. Huko, akapewa vyote ambavyo alikuwa akivikosa. Pesa, chakula kizuri na uhuru. Juu ya hayo, yakaja mafunzo. Hakuwa peke yake, walikuwepo mabinti wa nchi nyingine. Wenye rika ama makamo yakumfananishia. Wote kutokea nchini Dubai walipokuwa wakitumikishwa kingono. Nyoyo za wasichana hawa zilikuwa zimekufa. Walipofundishwa namna ya kuzitoa roho za binadamu wenzao, walifurahia. Muhimu vile ambavyo walidumu kutokuvipata, walivipokea walipovihitaji. Walifunzwa kila kitu kuhusu ulimwengu.

Kisha, wakavishwa taji la utukufu. Walihakikishiwa kuwa wameshatoka kwenye utumwa waliokuwemo, na sasa ni zamu yao kuwatumikisha wengine. Ni zamu

yao kuwa ma-Madame. Lakini wao, kwa kuwa hadhi yao ni kubwa zaidi, basi kila mmoja aitwe 'El Madame!'.

Jukumu likawa, kila mmoja kati yao, aende nchini kwao alipotokea, akatafute binti mwenye umri ambao haujafika miaka kumi na nane. Aingizwe kwenye mpango mzito sana wa kutengeneza wauaji wa kukodishwa duniani. Wauaji wenye umri mdogo. Wauaji wasiofikirika kirahisi kuwa ni wauaji. Na mradi huo ungekamilika, basi kila El Madame akaunti yake ya benki ingesoma tarakimu za kuthubutu kutamani kununua kisiwa ili afugie tu njiwa.

Yeye alipofika Tanzania. Akaelekea kwa nduguye, Magomeni. Maeneo ambayo watu wengi wenye asili ya Tanga na Zanzibar huishi. Lengo amsalimie tu, ili aendeleze safari yake ya kwenda Tanga—kumtafuta binti wa kumpeleka Italia.

Hamadi! Macho yake yanakwaana na almasi aliyokuwa akiitafuta. Alimuona Maya. Akaingia katika matamanio ya kumuweka kwenye mipango yake.

Yanini kuhangaikia panga na nyama yakatika kwa kisu?

Tiketi ya Tanga ikafia hapo. Akaweka mikakati mipya iliyomuingiza binti huyo wa familia ya kimasikini mtegoni. Wakambeba. Moja kwa moja Italia.

Baada ya miaka miwili, binti anatoroka.

Mwiba huchomoka ulipoingilia, akagundua kabisa hakuna pengine kwa binti huyo kukimbilia zaidi ya kurejea nchini alipotokea. El Madame wa Maya naye akarudi Tanzania. Akaunga mkia.

Upelelezi wa kumsaka Maya unamfikisha mwanamke huyu kwa Inspekta Kashmiri. Anampa ujumbe wa Maya. Na asubuhi ya kesho yake, anafunga safari mpaka kweye mahabusu ambayo Maya alishikiliwa. Lengo kumchukua Maya. Kufika kwenye korido. Uso kwa uso tena na Inspekta Kashmiri.

Akaona asichelewe sana, akamnasa mwanaume huyo na kuondoka naye. Akiwa na hakika kabisa Maya atahangaika kuja kumnasua.

Mtego!

# 13

Alipoifikia ile kona ya korido ambayo aliwaona wakikatiza, Maya hakumkuta yeyote wala dalili ya kuwepo mtu. Hakujua walipopotelea.

Kwa mbali sana, masikio yake yenye mafunzo ya kusikia kuzidi binadamu wa kawaida, yakaanza kupokea sauti hafifu ya hatua za watu walio katika mwendo wa kukimbia. Hisia zake zikamweleza kuwa ni polisi. Naye hakutaka kufanya uzembe wowote, akachukua jitihada za makusudi kukificha kiwiliwili chake.

Zilivyosogea dakika kadhaa za utulivu, akajitokeza. Lengo atoke. Lisingekuwa zoezi rahisi, pia kubaki ndani ya kituo halikuwa chaguo lake la wakati huo. Hivyo hakuamua kutoka nje, kwani, alijiingiza katika fikra na taratibu za askari polisi. Taratibu anazozitambua.

Mara nyingi, linapotokea tukio lolote kama lile, basi kituo ama gereza huingia kwenye kizuizi. Hakuna wa kutoka, hakuna wa kuingia. Fikra za Maya zikakimbilia

kwenye maegesho ya magari. Alilitafuta eneo hilo na kulipata. Akanyata taratibu na kuuchaguta uvungu mmojawapo, kisha akajivuta chini na kujitunuku hifadhi ya muda mpaka pale gari hilo lingekuja kuondolewa. Huku nyuma akawaachia askari purukushani na hekaheka za kutokwa na jasho mpaka kwenye meno.

Tofauti kabisa na Inspekta ambaye aliwekwa ndani ya utulivu katika siti ya kando mwa dereva. Taswira iliyokuwa kwenye mboni zake ni ileile ya siku moja iliyokuwa imekatiza. Isipokuwa tu, ilikuwa kinyume chake. Binti aliyekuwa akimuendesha, leo yeye amekuwa dereva. Hakuna ambaye alimuongelesha mwenzake. Kinywa cha msichana ambaye alikuwa akiuzungusha usukani kilishamdondoshea bonge la angalizo. Ni hilo angalizo ndilo lilimtundika Kashmiri Kashmiri katika gundi ya ukimya na unyenyekevu.

"Sina nia ya kukujeruhi, lakini, ukizungumza chochote kabla sijakuongelesha, au ufanye lolote litakalokwenda nje ya malengo yangu, mama yako na mkeo wapo kwenye kijiji ambacho juzi tu, mwenyekiti alizindua mradi wa pili wa maji safi!"

Hii ilikuwa ni kauli ya mtekaji kumuonesha Inspekta kuwa nafahamu ni wapi vilipo vipenzi vyako. Na kwa kuwa ilitanguliwa na maneno ya kuonesha hawezi kujeruhiwa, akadumu kuwa mtiifu.

Safari ya kibabe iliendelea kupamba moto. Inspekta Kashmiri hakuthubutu hata kujikuna ili kufanya jitihada za kujinasua. Aligusiwa kuhusu mama, akatajiwa mke, watu wake muhimu kabisa kwenye maisha. Hakutamani wadhurike. Kinywa chake kikabaki katika utiifu na kiwiliwili kwenye utulivu.

El Madame hakuwa ndani ya utani wala masihara. Alizichambua barabara za kulia kwa kushoto kama ambavyo alitoroka na Inspekta kule gerezani. Alimuonesha Inspekta kuwa naifahamu ofisi unayoifanyia kazi zaidi ya wewe unayekuja na kuondoka kila iitwayo siku.

Ghafla, sura ya mwanamke huyu ilibadilika ghafla baada ya masafa fulani.

"Tunafuatiliwa!" Aliongea huku macho yake yakitazama kwenye 'side mirror'. Inspekta akataka kugeuza shingo yake, akapigwa kwenye paja na kukatazwa.

"Usigeuke! Hapaswi kujua kuwa tumejua! Tazama kupitia kioo cha pembeni hapo. Unakuwa Inspekta wa namna gani wewe?" El Madame alizungumza kwa ukali.

Akili za Kashmiri Kashmiri wala hazikuwa zake kwa wakati huo. Mashaka ya kutekwa. Wasiwasi wa mama yake na mkewe kujulikana walipo, vyote vilimpokonya uzima wa ubongo wake.

"Hawa sio polisi wala wazoefu. Kasi yao ya gari haiko katika kiwango sahihi. Si kasi ya kumfuatilia mtu. Ni wahuni tu. Unaweza kuwajua Inspekta kabla sijawachezea mchezo mchafu?" El Madame aliuliza kwa kujiamini. Bado gari lilikuwa ndani ya mwendo. Akalisimamisha.

*******

Kwanza ilitangulizwa tamaa. Pesa iliwekwa mezani. Pesa ndefu. Kibopa kutokea nchini Afrika Kusini alilihitaji eneo katika mtaa wa Magomeni. Eneo

linalomilikiwa na mstaafu kutoka kwenye utumishi wa serikali.
Kwa kiwango cha zaidi ya milioni mia tano zilizowekwa kwenye macho yao, wale wenye mamlaka waliozipokea wakaihesabu ni kazi rahisi.
Akatumwa mwakilishi kwenda kuulizia bei ya nyumba hiyo, mwakilishi akarudi na jibu la nyumba kutokuuzwa.
Jibu la dharau!
Walilihesabu hivyo. Wakayatanua makucha yao na kukidhihirisha kiburi. Wakataka wamuoneshe huyo mmiliki wa hiyo nyumba kuwa ni wao nd'o wenye mbawa, hivyo wana uwezo wa kuzitanua juu ya yeyote wamtakaye. Hawakujali kuwa mamlaka waliyopatiwa ni kwa ajili ya kuwatumikia wale waliokuwa wameamua kuwaonea.
Wimbi la pili la bahari yao likaenda kwa vitisho zaidi. Wakiwa wameandamana na mjumbe wa mtaa ambaye walimpoza kiwango kisichozidi milioni tatu. Akaelezwa hiyo ni ya kuufunga tu mdomowe. Ipo nyingine ambayo kama zoezi lingekamilika, basi lingekuwa juu yake jukumu la kuchagua. Ale maisha,

au maisha yamle. Vyovyote vile, pesa ingekuwa ikizungumza badala yake.

Mjumbe akawa shuhuda namba moja namna raia wake wakitakiwa kuhama ndani ya siku chache kwenye nyumba yao halali, tena bila ujira wowote wa fidia.

Bado wahusika, wamiliki wa nyumba, hawakuonekana kutishika. Hata wakafikia kupigana nao vikumbo ndani ya ofisi zao kwa kile walichokuwa wakikizungumza kuwa ni haki itafutwayo.

Kesi ya nyani ilikuwa ikipelekwa mikononi mwa nyani wenyewe. Na kila kipengele cha anayedai kilivyosomwa kwa sauti, nyani walikiri kuwa wanachofanya ni uonevu. Lakini bado hawakukubali.

Uamuzi mzito ukafanyika. Mwenye nyumba auwawe. Vijana watatu wakatumwa kazi ya kwenda kuondoa roho ya mtu usiku wa manane. Na walifanikiwa kuingia mpaka ndani, mpaka kitandani. Walimkaba mwanaume, kama ambavyo walikuwa wameagizwa. Walielezwa mwanamke aachwe. Lakini kukurupuka kwake kutoka usingizi ndiko kuliponza. Katika kumtuliza, wakamchoma visu vya machoni na

kukimbia. Juu ya kitanda wakabakizwa majeruhi mmoja na mwili wa kiume ambao roho yake waliipangusa.
Vijana wakapewa chao. Maisha yakaendelea!
Wakaamini tayari yamekwisha. Baada ya miaka miwili inawafuata taarifa ya mmoja wao kupokonywa uhai. Hawajakaa sawa, simu inapigwa kutoka kwa mwajiri wao wa miaka hiyo, mwajiri akiwatahadharisha kuondoka haraka sana mjini ikiwa wanazithamini pumzi zao.
Kwanini?
Walihoji. Jibu waliloelezwa likawaacha hoi baada ya kuambiwa ni binti wa miaka kumi na sita ndiye aletaye kizazaa. Binti ndiye anayefanya mauaji. Tena mpaka muda huo tayari ameshamalizana na watu watano wenye kuhusika na uonevu pamoja na mauaji ya baba yake. Vijana wakaelezwa kuwa binti yupo gerezani. Na huko aliko, anaweza kufunguka mengi. Wao wakaona kukimbia ingekuwa ni katika kuliongeza tatizo badala ya kulitatua. Wakamtafuta askari aliyekabidhiwa faili la kesi husika, wakafanikiwa kumpata. Hatua ya kwanza waliyoamini ni sahihi kwao, ni kumfuata

nyumbani kwake. Wakafanya uvamizi. Lengo walipate faili la kesi na kujua kilichomo ndani humo, yakiwemo yale ambayo binti angekuwa amefunguka.
Na walipolikosa, wakaondoka na kumuacha askari na mkewe wakiwa hawajawadhuru. Waliamini hivyo, kuwa hawajamuathiri yeyote.
Siku nyingi zilipokatika, wakakata shauri la kuingia gerezani, ili kuhakikisha huyo binti aliyeshikiliwa wanamalizana naye akiwa ndani hukohuko. Wakaweka sawa mipango yao.
Ilipobisha hodi siku ambayo waliidhamiria, wakiwa nje wakijifikiria, wanaumuona yule askari ambaye waliwahi kufika kwake, akiongozana na mwanamke, wakaingia katika gari katika namna ambayo waliitilia mashaka.
Uamuzi ambao wao waliuona ni bora zaidi, ni kuwafuatilia wawili hao!!!
Baada ya dakika nyingi za mnyororo wao wa kuvuta mafuta, gari ambayo iliyokuwa mbele yao, iliyobeba wahusika wanaowahitaji, ikafunga breki. Na wao wakaisimamisha ile ya kwao.
Walikosea sana mas'kini ya Mungu!!!

# 14

"Koplo, leo nakufundisha kitu ambacho katika madarasa yenu ya kipolisi, hamkuwahi kabisa kukisoma," El Madame alizungumza. Alikuwa amevaa gauni refu, jeusi, lenye maua ya bluu yaliyojipanga kwa uzuri kabisa.
"Ni Inspekta. Inspekta, sio Koplo!" Inspekta Kashmiri akairekebisha kauli ya mwanamke huyo.
Macho yake yakiwa bado yameganda katika 'side mirror', El Madame aliendelea kuzungumza, "Okay. Inspekta. Ni hivi, kamwe ukishamtambua adui yako ni nani, hakikisha hauanzi kumsogelea. Usianze wewe kumshambulia. Kwenye mapambano, jitahidi uwe unafuatwa wewe. Ili hata ukitoa kibano, Mungu na Malaika wake watashuhudia kuwa hukufanya uonevu."
Inspekta Kashmiri alimsikiliza mwanamke huyo huku akimuangalia.

Uso wa El Madame bado ulikuwa katika kioo kulitazama lile gari.
"Unahitaji nini kutoka kwangu?" Inspekta akavunja kanuni ambayo aliwekewa tangu awali. Alielezwa kabisa, hakutakiwa kuzungumza lolote ambalo hajaulizwa.
"Namhitaji Maya Inspekta!" El Madame alimjibu huku akiutegua mkanda wa siti. Kisha akaongea jambo huku akitabasamu, "Inspekta, wanaume wawili wanakuja. Mmoja anaonekana ni mtu wa mazoezi. Mwingine, aliyekuwa nyuma yake, ana wasiwasi. Macho yake yanaonesha ndani ya saa sita zilizopita amekunywa pombe. Sio kwa asilimia nyingi za kilevi, lakini hii inamfanya asiwe mtu kamili. Huyu wa mbele kidogo nitatumia nguvu, ila huyo mlevi ni pigo moja tu!" Alizungumza El Madame. Ni msichana aliyefunzwa mapigano. Kanuni ya kwanza kabisa ambayo hupewa watu wanaoingia kusoma mapigo hatari, ni kanuni ya kisaikolojia. Unapaswa umjue mpinzani wako kwa kumuangalia. Tena ndani ya sekunde chache.
Inspekta alisikia alichokuwa akielezwa, alipopindisha macho yake kuwatazama watu hao ili kuipata picha

kamili, anakwaana na sura ambayo iliwahi kupita katika kitabu cha maisha yake.

Iko ukurasa wa ngapi hii sura?

Labda alijiuliza.

Ila, ilipozidi kusogea kwa karibu, akagundua ilikuwa katika ukurasa wa kisasi. Ukurasa usio na namba. Ilikuwa ni sura ya Gwaya. Mtu aliyemfanya mpaka akairudia kesi nzito kiasi kile iliyomuingiza matatizoni.

Mwanzo kabisa, Inspekta aliombwa utulivu kwa ahadi ya kutakiwa kupewa darasa. Unadhani aliweza sasa?

El Madame hakujua ni kwa wepesi upi, lakini alikuja kushtuka mtu wa pembeni yake ameshaufungua mkanda wa siti.

Hamjamgusa amzuie, tayari ameshakamata loki ya mlango na ameshaitekenya, mguu mmoja uko nje!

Inspekta Kashmiri amegeuka mbogo. Kiuononi hakuwa na bunduki wa silaha yoyote. Lakini nguvu ya uchungu wa kumpoteza mtoto ndiyo ilizisukuma nyayo zake kuzipiga hatua. Hatua kumi na moja.

Gwaya huyu hapa mbele yake!

Bila mpangilio, kwa hisia tu, bila hesabu, bila makadirio, Inspekta anachomoa ngumi kuipeleka kwa Gwaya. Akiidhamiria taya.

Gwaya anainama kidogo tu, kidogo sana, mkono wa Inspekta unapangua hewa. Ngumi inakwepwa.

Ubavu wa Inspekta uliobaki wazi, ukawa mbele ya uoni wa jamaa aliyekuwa ameinama...

Atake nini tena Gwaya?

Naye akachanua ngumi yake iliyopaswa kwenda kuvurugua vitu vingi kwenye tumbo la Inspekta. Lakini ikadakwa. El Madame alishaingia mchezoni. Tayari alishashuka kutoka garini! Ile ngumi iliyokuwa imedakwa, bado iliendelea kushikiliwa, mkono ukaminywa, ukazungushiwa katika kiwiko. Mwendo wa kiwiko ni wa kupanda ama kushuka, wakati huo, kiliingizwa katika mwendo mpya kabisa kibaiolojia, kikapelekwa kulia kwa nyuzi mia tatu. Gwaya akahisi mifupa yake inamegeka kama mua mtamu uliowekwa katika goti la mlaji aliyekosa kisu cha kugawanyishia.

Yowe likamtoka!

Binadamu, wa kawaida, ili upige kelele, lazima utawanye mishipa ya koo, ni hili koo ndilo ambalo El

Madame aliliona kwa wepesi zaidi, akaligonga kwa ncha za vidole vyake! Kelele zikakata bila ya ridhaa ya aliyekuwa akizitoa. Gwaya akabaki katikati. Akohoe au atafute pumzi iliyokuwa ikiingia katika mrija wake wa hewa kwa tabu. Akadondoka chini na kutapatapa. Ndani ya sekunde kumi na tano, Inspekta Kashmiri alishuhudia mbaya wake akipoteza uhai.

Sasa akabaki yule wa nyuma. Yule ambaye El Madame alisema amekunywa. Kwa muziki aliokuwa ameushuhudia, kwa suluba aliyofanyiwa mwenzake mbele ya macho yake, akageuza mgongo akimbie. El Madame hakumwacha!

Alibinuka sarakasi tatu za hewani, za haraka, ak'enda akatua mbele yake...

Ghafla, makofi yakaanza kupigwa! Makofi na mbinja za pongezi.

Tukio hili lilikuwa likitokea barabarani. Hadharani. Tayari umati ulishalizunguka eneo hilo ili kushuhudia. Wenye simu walitoa ili kuhifadhi kumbukumbu za picha. Wenye watoto wao wakawainua. Ili watazame ule mchezo wa kuigiza uliokuwa ukiendelea. Kila rika. Wazee kwa vijana. Wavulana na wasichana.

El Madame alipozungusha macho yake na kuona hali hiyo, hakumfanya kitu yule mlevi. Alimwacha. Alikimbia mpaka kwa Gwaya aliyekuwa amemdondosha. Akampekua mfukoni na kumchomolea simu yake. Kisha akamfuata Inspekta na kumkabidhi.

"Twende! Hatuna muda tena!!" Inspekta Kashmiri alishikwa mkono kwa nguvu na kupelekwa kwenye gari. Milango ikafungwa, safari!

'Eh bwana eeenh, michezo ya siku hizi bwana! Kama kweli vile!! Sema Bongo muvi imebadilika!'

Hii ilikuwa ni sauti ya kiume iliyokuwa imevutiwa na tukio. Ikiamini ni sehemu ya maandalizi ya filamu ama igizo. Mambo ya namna hiyo ni adimu kutokea katika nchi yenye uwenjeji wa amani na utulivu kama Tanzania.

Wachache waliobahatika kuumbwa na ujasiri katika nyama za vifua vyao, wakaweza kusogea. Walifika mpaka kwenye ule mwili. Kila wakigeuka kusubiri kukatazwa, kimya!

Hamna hata anayekoroma!

Akili ya kutafuta kamera zilipo, ikawajia.

Papasa kwa macho na kupapasa weeh, kweupe. Basi wakashauriana wamwamshe, kwamba, labda wenzake wamemsahau!

Kimyaaa! Kidole cha shahada kikalazwa katika tundu za pua yake, kwa baridiiii! Hakuna ujoto. Kumaanisha kuwa hakuna hewa inayotoka. Na kama hakuna kinachotoka, basi hakipo kinachoingia. Hiyo ndiyo kanuni ya ulimwengu na uhai. Hivyo, mtu yule hakuwa akivuta pumzi ndani.

Kifo! Mtu kafa! Maiti! Mtu kauwawa! Mauaji!

Kila mtu alitumia neno lake wakati akikimbia kupoteza ushahidi. Wale watoto waliokuwa wamepandishwa kwenye mabega watazame, sasa waliwekwa chini ili waangalie ustaarabu wa kupambana na hali zao.

Ikawa ni zamu ya taarifa kutembea kwa kasi. Mwenye bajaji akamtonya mwendesha pikipiki. Naye akalifikisha kwa dereva wa daladala...

Dereva naye abaki nalo la kazi gani?

Akalitupa kwa konda wake. Huyu sasa akawa muuzaji wa mwisho. Muuzaji wa rejareja. Alilitoa kidogokidogo kwa kila abiria aliyemrudishia chenchi ama kumkabidhi tiketi...

Hilooo! Likatua katika ofisi ya kahawa iliyo karibu na kituo kikubwa cha polisi. Askari waliokuwa wakipata kifungua kinywa wakazisikia hadithi za mwanamke mwenye kupigana kama nyota wa filamu za kichina!

Mwanamke? Tena kaua?

Kule gerezani kukalipuka. Wakahisi mtuhumiwa wao waliyekuwa wakimtafuta, aliyetoroka, Maya, ndiye aliyeleta varangati hilo. Wakaona hako kabinti kamaenza kuwazoea na kuchupa mipaka. Kikosi kazi kikaandaliwa. Magari yakawashwa...

Yakatolewa na mengine yaliyokuwa maegesho....

Hapa kwenye kuchukua magari hapa...

Hivi, walishindwa vipi kukagua uvunguni jamani? Au nd'o hiyo haraka?

Agh!

# 15

Himahima, gari ziliongozana kuliacha geti la gereza. Jicho la Maya lilikuwa likitazama lango hilo lilipokuwa likifungwa kwa nyuma. Alishikilia vyuma vya uvungu wa gari. Kitaalamu mno. Si kila mtu anayeweza kuning'inia chini ya uvungu wa gari. Gari yenye kutembea! Achilia mbali huo wa kitanda ambao ndani ya sekunde mbili tu ,mgongo wako unakuwa umeibusu sakafu!

Hapa nauzungumzia uvungu wa chombo cha moto kilicho kwenye mwendo! Kunahitaji utaalamu. Kunahitaji ujuzi. Kama aliokuwa nao binti huyo. Maya.

Ulikuwa ni msafara wa magari kumi, lile ambalo binti huyo alilidandia, lilikuwa ni gari la sita kutokea mbele. Alitamani kushuka, lakini mwendo wa madereva hao ulikuwa ni mkali kuliko kawaida. Waliwasha ving'ora pia, kuomba kupishwa, isingekuwa rahisi kusimama.

Labda Maya angejirusha, lakini uamuzi huo alishaelewa ni wa hatari zaidi, kujiachia kwake, kungepaswa kuwe kwa kasi zaidi, angetakiwa ajidondoshe chini, kisha ajizungushe kwa wepesi kutoka uvunguni. Wepesi wa kasi zaidi kuushinda mwendo wa matairi ambao kwa makadirio ni zaidi ya kilomita mia kwa saa. Isingewezekana. Angekanyagwa. Afanye nini sasa? Na anahitaji kushuka.. hataki afike mwisho wa msafara ule...

Ugumu uliokuwa kiunoni mwake, ugumu wenye uzito kwa mbali, ukamkumbusha jambo...

Kuwa, ile bunduki aliyompokonya Inspekta Kashmiri, akamtisha nayo na kumtoa mule chumbani, mule kwenye chumba cha mahojiano, bado yuko nayo...

Maya, akajivuta, kwa ujasiri, akaachia mkono mmoja kutoka kwenye chuma aliyokuwa amenasia. Halikuwa zoezi jepesi. Kijaso kilimtiririka. Changanya na lile joto kali la kumchemka kwa injini ya gari.

Aliichomoa ile bunduki, akaielekeza pembeni, pembeni kabisa, na kuiinua kwa juu kidogo, ili kuepusha madhara ya wasiokuwa na hatia, kisha akafyatua mshindo wa risasi. Mshindo mmoja tu!

Huu ukasikika hata na kunguru waliokuwa angani, wakawa wenye  kulalamika kutaka kujua ni kitu gani, askari wakaacha kuyavuta mafuta na miguu kuhamia katika breki. Gari zilisimamishwa. Lengo la Maya lilitimia.
Binti akautua mwili wake mdogo katika lami na kujizungushia pembeni. Kabla ya askari kushuka chini, yeye alishafika ng'ambo ya pil. Hapo akawahi katika njia yenye watu wengi na kupotelea kwenye msongamano. Polisi wakaanza kuhaha kutafuta mlio ulipotokea. Huko na huko hakuna walichokishuhudia. Fikra na matamanio ya kuvipindisha viuno vyao zikawajia. Watazame chini ya magari yao. Labda kuna tairi imepasuka.
Walipoangalia, ilikutwa bunduki. Ilionekana ni aina ya bunduki inayotumiwa na askari polisi. Wakaichukua. Wakaendelea na safari yao. Walipofika huko waliporipotiwa kutokea tukio, walikuta ramani za eneo ambao mwili ulidondoshwa. Ramani zilizochorwa na kitengo cha dharura cha polisi kilichokuwa kimewahi kabla yao. Waliohusika hawapo. Wakaomba watumiwe sehemu ya ushahidi ambao utakuwa

umepatikana na hao polisi waliokuwa wamewatangulia.

Wakarudi mikono mitupu...

Hapana! Haikuwa mitupu. Walirudi na ile bunduki. Bunduki waliyoiokota. Walipoipitisha katika tathmini za kiusalama, wakagundua ni jino la mamba anayelala katika bwawa lao. Ni bunduki ya askari mwenzao. Inspekta Kashmiri Kashmiri. Bunduki iliyosajiliwa kwa jina lake.

Haraka sana simu ya Inspekta ikapigwa, kuulizwa ni wapi alipo, ikibidi awahi kutoa maelezo, simu haikupokelewa. Iliita mpaka ilipokata yenyewe.

Zoezi liliporudiwa, wakisubiri simu ipokelewe... Wakapokea kile ambacho waliagiza awali. Zilikuwa ni sehemu ya picha zilizopatikana wakati lile tukio la barabarani likiendelea. Picha kutoka kwenye simu za raia. Wala halikuwa tukio ambalo lilifanywa na binti waliyekuwa wakimdhania, Maya. Laa hasha!

Mtendaji alikuwa mwingine kabisa. Lakini, macho yakanasa kwenye sura iliyokuwa jirani wakati tukio hilo likiendelea, sura ya mtu wamtafutaye, sura ya Inspekta Kashmiri Kashmiri!

Kwa mara ya pili, taa nyekundu ikamwakia. Haikuwa rahisi kwao kumuwazia vibaya, lakini jumba bovu la shutuma na mashaka lilianza kumuangukia afande huyu... Watu wakaanza kuunganisha nukta za mfululizo wa matukio yaliyotanguliwa na 'kwanini' za kutosha...

Kwa nini alikubali kiurahisi kuirudia hii kesi? Kwanini alihitaji kumuhoji mtuhumiwa ofisini kwake na sio kwenye chumba maalumu kilichotengwa kwa kazi hiyo? Kwanini tulivyoweka kinasa sauti kilizimwa? Kwanini leo limetokea tukio kubwa hivi na ameondoka? Kwanini anaonekana kwenye picha za mauaji ya kule barabarani? Kwa nini simu yake haipokelewi?

Na hakukuwa na jibu hata moja zaidi ya kusubiriwa ushahidi. Ushahidi juu ya harufu ya usaliti iliyoanza kufuka juu ya jina la Inspekta Kashmiri.

Ushahidi tu!

*******

Mtu wa Mwanza. Msukuma wa maamuzi na asiyeogopa chochote ikiwemo sheria. Mhalifu wa

kupindukia aliyewahi kufungwa karibu kila gereza lililopo kanda ya ziwa. Wachache wanamfahamu jina lake. Lakini wengi wakaridhika na lile walilokuwa wamelizoea. Ama tuseme kulisikia tu... Anazoeleka wapi?

Kaka Kubwa!

Hakuna kitu adimu katika uso wake kama tabasamu. Jambo la kumfurahisha mtu wa kawaida kufikia kuangua kicheko cha kugalagala, yeye angeonesha sehemu ndogo tu ya meno yake kisha angekifunga kinywa. Si mtu wa masihara. Hasa linapokuja suala la pesa mbele ya mjadala.

Yeye kufanya jambo la kikatili akiwa kwenye furaha ni kesi ya kawaida sana. Na asubuhi ya siku hiyo, alikuwa amevaa hasira. Mbele yake kulikuwepo mateka aliyekuwa ndani ya sare za kipolisi. Tangu amkamate siku ya kwanza, hakuwahi kumzungumzisha. Haikuwa sehemu ya kazi yake, na yeye si wa kufanya kile ambacho aliagizwa.

Alitumwa na Inspekta Kashmiri Kashmiri kumkamata askari huyo, akae naye kwa siku kadhaa ili aendeleze upelelezi wa kesi, na pale ambapo siku zingefika mbili,

basi angetumiwa pesa ya nyongeza, au angeambiwa amuachie...
Hiyo ilikuwa ni asubuhi ya siku ya tatu, hakuna lolote kutoka kwa muagizaji. Na kila simu yake ilipokuwa ikipigwa, hakupokea. Hili lilimkera Kaka Kubwa. Makubaliano ya pesa yalikuwa yakivunjwa. Dhambi asiyoipenda zaidi katika dunia ilikuwa ikitendeka. Tena dhidi yake. Aliamini ameanza kudharauriwa...
"Wewe!" Kaka Kubwa akamuita mateka aliyekuwa amemketisha mbele yake.
Mateka akainua uso. Ni mara ya kwanza alikuwa akiisikia sauti ya kiumbe huyo tangu alipokwapuliwa jioni ambayo alikuwa akitoka kazini.
"Nafikiria nikuue vipi, eti, niambie.. unataka kufa kifo gani?" Kaka Kubwa alikoroma akiutaja umauti kwa wepesi kabisa kama jina la kinywaji kitamu.
Yule askari mateka akaanza kuangusha kilio. Kilio cha hofu. Kilichokosa machozi. Hana cha kutoa. Alishayamwaga sana tangu alipotiwa kizuizini.
"Haya, kama hutaki kwenda kukijua kiza cha kaburi kilivyo, naomba unitajie namba za kiongozi wako wa kituo. Nina haja naye!"

Naam, jamaa alikuwa akihitaji namba ya kiongozi. Alitaka kumuonesha Inspekta Kashmiri vile wanavyotendewa wapuuzi wanaovunja makubaliano.
Yeye si kamwaga mboga? Alitaka kumfundisha kuwa ugali haumwagwi, unakanywaga ili usitamanike kabisa.
Lengo la Kaka Kubwa kuitaka namba ya kiongozi, ni kuripoti kuwa, yeye ni mtekaji aliyetumwa na Inspekta Kashmiri ili kumteka askari mwingine...
Tayari namba ilikuwa kwenye simu yake, na ameshaipiga, chombo kipo sikioni...
Hakika hii ilikuwa ni siku mbovu zaidi kwa Inspekta Kashmiri. Na hakuwepo Malaika wa kumuepua katika chombo ambacho kwa siku hiyo ulimwengu uliamua kumchemshia.

# 16

KILIKUWA ni kikao cha dharura. Ndani ya gereza. Wakuu wote katika vyeo nyeti walikuwepo. Hakuna ambaye alituma mwakilishi. Pengine kilikuwa ni kikao muhimu kuliko vikao vyote walivyowahi kuvifanya. Na kigumu vilevile. Maana, kilihitaji majibu mbele ya maswali yasiyowezekana.

Yalikuwa majira ya mchana, kwa ratiba ya kawaida ni muda wa askari polisi kwenda kupata chakula. Wakiwemo wale wenye vyeo vya juu. Lakini kwa siku hiyo hakuna tumbo lililothubutu kulalamika njaa.

Haikuwa mara ya kwanza mfungwa kutoroka katika historia ya gereza, ila kwa hali ya kuondoka huku akiwaacha baadhi ya walinzi wakiwa na majeraha, lilikuwa ni jambo la kufedhehesha lenye kuhitaji uwajibikaji wa haraka sana.

Kwanza lilisomwa faili la mtuhumiwa. Walikuwemo baadhi ambao hawakumjua Maya hasa ni nani. Taarifa

zikawekwa wazi. Wakatokea walioshangazwa. Kumbe hekaheka zote hizo ni binti tu wa miaka kumi na sita? Ikawachekesha baadhi. Wakaambiwa ili vicheko vyao viwe vitamu zaidi, aletwe askari mmojawapo ambaye upepo wa tukio ulimkumba. Alikuwa ni mmoja wa askari walioingia mule kwenye chumba cha mahojiano. Ni yeye pekee ndiye ambaye walau alikuwa akiweza kuzungumza. Akaletwa ndani ya ukumbi ambao kikao kilikuwa kikiendelea. Akiwa juu ya kitanda cha machela. Kiliburuzwa huku amelazwa. Uhusiano mwema kati ya pingili za mgongo wake na nyonga ulishavunjwa. Hakuweza kuketi kwa makalio.

Ni huyu ndiye aliyetoa maelezo kuhusu kile alichokishuhudia. Akasema kama ingekuwepo nyundo, basi ni bora angetandikwa nayo ya utosi lakini sio ngumi ya binti huyo. Maelezo yake yalikuwa mengi, akieleza kile alichokishuhudia na ambavyo alisikia. Akidai ndani chumba hicho ni kama walikuwa wakipigana na wanajeshi kumi wenye silaha. Mwisho kabisa akabaki akilalamika taya zinamuuma hivyo asingeweza kuendelea kuzungumza. Shuhuda huyu akatolewa ukumbuni.

Vile vicheko vyote vikayeyuka. Waliokuwa wakihisi ile taarifa ni ya mzaha, wakarekebisha mikunjo ya viwiliwili vyao ili wakae vizuri kuusikiliza mjadala na kupata hitimisho.

"Huu sio uvamizi wa kijasusi?" Wachache wakajaribu kuhoji. Uvamizi wa kijasusi, hutokea pale ambapo, mpelelezi wa Taifa moja, anakwenda kufanya harakati zake katika Taifa lingine. Walianza kuhisi Maya ni jasusi aliyepandikizwa kutoka kwenye nchi nyingine.

"Hapana. Sio rahisi!" Mwingine akajibu kulingana na hoja za kichwa chake.

"Na hakuna kati yetu anayeweza kuthubutu kusema uvamizi wa kijasusi ni jambo rahisi!" Mtoa hoja wa mwanzo akatia uzito.

Mapendekezo kadhaa yakatolewa. Kesi hiyo ilipaswa kufikishwa katika jeshi. Ili upelelezi wa juu zaidi uendelee. Na kiutaratibu, taasisi hizi mbili haziingiliani kiutendaji. Kesi inapotoka mikononi mwa polisi, ndiyo imetoka. Walikuwa wakiamini kwa ngazi hiyo, zipo hatua za kiintelejinsia zaidi zingechukuliwa. Pendekezo lingine, akatakiwa apatikane askari anbaye alikuwa akihusika katika upelelezi wa kesi hiyo. Maelezo yake

yangekuwa muhimu zaidi. Kwani, bila shaka ndiye ambaye angekuwa amefanya mahojiano na mtuhumiwa.
Yuko wapi?
Waliulizana. Ikatolewa taarifa iliyokuwa imejaa cheche zenye kuonesha kuwa mshukiwa wa kwanza wa tukio lililojiri, ni yeye. Mtu waliyetegemea aje kuwapikia mtori, ndiye aliyeukata mgomba ungali haujakomaa. Ndizi zingepatikana wapi?
Ilitamkwa kwa jumla kuwa ni kushukiwa tu. Ushahidi wa hilo haukuwepo.
Simu ya mmoja aliyekuwa ndani ya chumba hicho cha mkutano ikaita. Ndiye aliyekuwa mkuu wa kituo akifanyiacho kazi Inspekta Kashmiri Kashmiri. Aliitazama simu hiyo ilipokuwa ikiita mpaka ilipokata yenyewe. Haikuwa na mlio.
Baada ya dakika tatu, akaomba ruhusa ya kwenda chooni. Hakuwa na haja, alikwenda kwa lengo la kuisikiliza simu hiyo akihisi inaweza kuleta taswira mpya yoyote juu ya kesi iliyokuwa iking'ong'a vichwa vya wengi.

Fikra zake zilikuwa sahihi. Alipopokea tu simu, swali likatoka upande wa mpigaji...

"Nazungumza na bosi wake Inspekta Kashmiri?"

Akapata shida kujibu. Alinyamaza akijaribu kuitafakari ile sauti mbaya kiasi kile ni ya nani!

"Oyaaa! Nazungumza na bosi wake Inspekta Kashmiri?" Swali lilirudiwa.

"Ndiyo," akajibu kwa utaratibu akihakikisha kama kuna yeyote nje ya choo kile asiweze kusikia.

"Jibu hivyo! Sio unakaa kimya kizembe! Haya, ninataka kuongea na wewe jambo kuhusu askari wenu!" Kwenye simu kulifoka. Mkuu alianza kuhisi kama kuna mdomo ulitaka kutoka kuling'ata sikio lake. Kwa namna sauti hiyo ilikuwa si ya kupendeza.

"Sawa!" Akaitikia.

"Askari wenu, Inspekta Kashmiri, alinipa kazi, nimteke askari mwingine. Sijui ni kwa malengo gani, lakini tambueni hilo. Sasa huyu askari niliyemteka, nitamuacha kwenye ukuta unaouzunguka uwanja wa CCM Kirumba, dakika ishirini zijazo. Huyo aliyenituma amevunja makubaliano, na mimi siwezi kumfichia maovu haya. Ahsante!"

Simu ikakatwa. Yule mkuu akatoka mkukumkuku chooni na kukimbilia kwenye chumba ambacho kikao kilikuwa kikiendelea. Kwa namna ambavyo aliingia, watu wote wakabaki kimya wakimtazama yeye.

Na hakusita, alifungua kinywa chake, akazungumza yale yote aliyoelezwa kwenye simu. Chumba kikabadilika, kikawa ni kitengo cha dharura cha mawasiliano ndani ya muda mfupi. Vyombo vya usalama vya mkoani Mwanza vilitafutwa. Vikapewa habari na maagizo ya kuwahi haraka eneo la uwanja wa CCM Kirumba. Ikibidi walizunguke kabla ya dakika ishirini zilizokuwa zikifuata. Walihitaji kuwapata wote wawili. Huyo aliyekuwa akijiita mtekaji wa kuagizwa, na aliyetekwa mwenyewe.

Dakika kumi mbele, simu ya yule Mkuu wa Inspekta, inaita. Kwa namba ileile, anaamua kuipokea akiwa mule chumbani na kuiwekea kipaza sauti. 'Loudspeaker'. Nia, kama ni ushahidi, basi usikike na kila mmoja.

"Nimekwambia baada ya dakika ishirini, naona umekuja baada ya dakika tano... Hivi nyie mkoje? Mbona hamsimamii makubaliano?" Sauti ya mpigaji

ililalamika kwa namna ya kugombeza. Askari hakujibu kitu, alihitaji mtu huyo aendelee kuzungumza zaidi..

"Okay. Mtu wenu nimemuacha nilipowaeleza. Kwa heri!"

Simu ikakatwa. Wengi wakahisi kuna mchezo ama mzaha uliokuwa ukifanyika kuwatoa kwenye reli kuhusu kutoroka kwa binti Maya.

Kabla ya kupata mapumziko, simu ya kipolisi kutoka Mwanza ikaingia. Ni kweli, ilikuwa ni taarifa kutoka katika ukuta wa uwanja wa CCM Kirumba. Kulikutwa mtumishi wa jeshi akiwa ametelekezwa hapo huku amefungwa.

Yule mpigaji akaaminiwa. Na alipopigiwa, hakupokea. Baada ya muda akawa hapatikani kabisa. Huu ukawa muhuri rasmi katika karatasi iliyojaa shutuma kumhusu Inspekta Kashmiri. Ikahitimishwa kuwa amehusika.

Sasa yuko wapi?

Walijiuliza. Wakiamini, wakimpata yeye, basi wamempata na huyo Maya. Walihisi, sababu ya Inspekta Kashmiri Kashmiri kumteka askari mwenzake,

ilikuwa ni kuhakikisha zoezi la kumtorosha Maya linafanikiwa.

Ukatangazwa msako mkali wa kumshika Inspekta Kashmiri Kashmiri popote alipo! Bila kujua kuwa, kuna mikono iliyokwisha kumuweka kizuizini.

Huo ukawa mwanzo rasmi wa hekaheka.

# 17

Ulifanyika mzunguko mkubwa wa mshale mrefu wa kihesabu majira, saa moja na dakika ishirini, mpaka alipofika Magomeni Mapipa. Maya alikwenda moja kwa moja anapoishi mama yake. Akaelezwa kuwa amelala. Binti huyu mwingi wa adabu hakutaka aamshwe. Akaketi na Benard, wakawa wanazungumza. Benard, ndiye mtu pekee katika ulimwengu huu na usiokuwa huu, kama upo, anayeweza kuketi na msichana huyo, wakaingia katika maongezi ya kawaida. Huyu Benard ni nani?
Siku ambayo zoezi la Maya la kutoroka nchini Italia lilipofanikiwa, alipanda ndege na kurudi Tanzania. Moja kwa moja. Kule ambako alikimbia kwa kuvizia umakini wa ulinzi uliopungua kidogo, binti huyu aliweza kuchukua pesa ya nauli kidogo. Na ilitosha kwa nauli pekee. Hakubeba kiwango kingine cha ziada. Hali iliyomfanya kuwa mshangaaji baada ya kutua

kwenye uwanja wa kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Hapo, Maya alihitaji usafiri, lakini, hakuwa na hata thumni katika uzito wa mfukowe. Akatumia mbinu ya kutia huruma. Akiamini kwa umri wake mdogo, lazima tu angetokea wa kumpa msaada.

Aliposegeza kiwiliwili chake kwa mtu wa kwanza, aliyekuwa mwanamke, jinsia tunayoelezwa ndiyo wakina dada, shangazi na mama wa kulea, kuwatunza na kuwakuza watoto wadogo, alitazamwa kuanzia juu mpaka chini. Kisha akasonywa kwa kubetuliwa mdomo bila ya kupewa jibu lolote.

Nyuma ya msichana huyo alikuwepo mvulana. Huyu mavazi yake yalichoka. Maya alipomtazama, aliamini asingeweza kupewa msaada naye. Hakumuongelesha.

Ajabu, mvulana ambaye alikuwa ameshika mabegi, alimuita Maya kwa kunong'ona...

"Binti... Una shida gani?" Aliuliza mvulana huyo. Usoni mwake palijaa tabasamu lenye wasiwasi.

Wakati yeye akiamini anazungumza na msichana mdogo asiyeelewa chochote, Maya alishatambua mpaka chanzo cha ile hofu katika mashavu yake yenye

kutikisika. Kuwa jamaa huyo ni mfanyakazi tu. Na yule msichana aliyekuwa mbele yake huku amekamata simu mkononi, ni bosi wake.
"Nauli..." Maya alijibu kwa kumridhisha. Akitumia sauti ileile, ya chinichini.
"Unaenda wapi?" Mvulana aliuliza. Bado alikuwa makini akimtazama bosi wake mbele. Na hakusimama.
"Magomeni Mapipa!" Binti akajibu.
"Okay, nifuate... Kuwa karibu na mimi!" Yule mvulana alitoa agizo.
Maya akaunga hatua zao. Hakujua msaada aliokuwa akienda kupatiwa. Alichokuwa akikihitaji binti huyo kwa nyakati hizo ni nauli tu. Achilia mbali kuhusu lile tumbo la njaa lililokuwa likimsokota. Hilo aliliweka kando ya mazingatio yake.
Kufika kwenye gari, yule msichana, yule ambaye Maya alimzungumzisha kwa mara ya kwanza–akamsonya, yeye aliingia kwenye siti ya mbele. Kijana, mfanyakazi wake, na dereva pia, akamfungia mlango. Kisha mapema sana akarudi nyuma na kufungua eneo la kupakiza mizigo, kwenye buti, akamueleza Maya apande kwa haraka. Akimuahidi wanapita karibu na

huko anapoelekea, hivyo, angemshusha. Kwa namna yoyote ile.

Na ikawa ambayo iliahidiwa, karibu na maeneo ya Magomeni, huyu kijana aliigiza gari kupamepata matatizo. Akaisimamisha. Ili tu kulitimiza lengo lake la kutoa msaada, akarudi chapuchapu nyuma na kumfungulia Maya. Akimwambia binti huyo aondoke mara moja.

Maya alimshukuru. Kabla ya kutii aliloamuriwa, akaomba kitu kimoja. Aliomba alijue tu jina la binadamu yule mwenye roho ya utu ni lipi. Kijana akitazama huku na huko kwa wasiwasi, alijibu, "Benard!"

Huu ukawa mwanzo wa wawili hawa kukutana. Na hakuna hata mmoja kati yao aliyetegemea wangekuja kuonana tena!

Siku ambayo Maya aliingia katika nyumba ya kiongozi wa serikali. Masaki. Kiongozi fedhuli na mbaya wa kutumia madaraka. Ambaye alishiriki katika kuwadhulumu nyumba yao. Binti huyu hakuna ambacho alikwenda kukifanya tofauti na mauaji.

Alitaka kulipa roho ya baba yake iliyotolewa pasi na haki.

Alipokuwa akitoka, baada ya kukamilisha kazi, akakwaana na mlinzi.

Ilikuwa ni usiku, lakini eneo hilo lilienea mwanga wa kutosha. Mwanga wa taa. Nyuso za wawili hawa zikawa zenye kutazamana. Yule mlinzi hakuelewa cha kufanya. Ni kama alibebwa na jinamizi la bumbuwazi.

We' binti, umefikaje hapa?q

Labda kinywa kilichokuwa kimya cha mlinzi kilitamani kunena hayo. Lakini ule ubaridi wa kuifananisha sura ukamzuia. Kuja kukaa sawa, Maya ameshafanikiwa kumpotea.

Hii ilikuwa ni mara yao ya pili kukutana. Maya na Benard. Benard akiwa ndiye mlinzi wa nyumba hiyo. Nyumba ambayo Maya alitoka kufanya mauaji.

Miezi miwili ikakatika. Maya akiwa katika mazingira ya mtaa wao ikawa zamu yake kukutana sura anayoifahamu. Ikiwa katika mazingira magumu mno.

Kumsogelea vizuri, ni Benard.

Wawili hawa ikabidi waketi wazungumze.

Sawa, milima haikutani na bindamu wenye miguu nd'o wamejaaliwa hilo... lakini nd'o kila mara?

Hapana! Pengine lipo kusudi katika hilo!

Wakatafuta mgahawa, awamu hiyo ile ihsan ambayo Benard aliitoa ikawa inamrejea kwa namna nyingine.

Benard alieleza kuwa, usiku ule, bosi wake aliuawa. Hivyo, ndani ya mwezi mzima yeye kama mlinzi alitupwa rumande ili kupisha uchunguzi ufanyike. Upelelezi ulipokamilika na kugundulika kwamba hakuhusika, akatolewa. Na huo ukawa mwisho wa kibarua chake. Limbikizo la mshahara wa miezi miwili alilokuwa akilidai likawekwa kando. Akafukuzwa.

Mjini hana ndugu yeyote wa kwenda kumlilia hata bilauli ya maji ya kunywa. Akabaki kutafuta vibarua vidogo vidogo, walau apate nauli ya kurejea nyumbani kwao, kijijini. Kwa mama yake aliye mlemavu wa miguu yote, na baba yake kipofu.

Simulizi hii ilimtoa machozi Maya. Benard akazivaa hisia na kumtazama yule msichana kama mtoto mdogo mwenye ukomavu na uelewa mpana. Akashawishika kumsaili kuhusu maisha yake, likiwemo

lile alilolifuata siku ile usiku kwa bosi wake. Usiku ambao mauaji yalitokea.

Ni hapo, ndipo, Maya akafungua ukurasa mmoja wa uaminifu. Mmoja tu. Kwani katika masomo ya kijasusi, wamefunzwa kuwaheshimu watu wasiowafahamu na sio kuwaamini. Walakini, mvulana huyo aliyekuwa mbele yake, ndiye aliyempa imani siku ya kwanza kabisa aliporejea Tanzania. Imani ya kupewa msaada.

Maya akaona isingekuwa dhambi kulirudia jambo hilo. Akamtamkia historia yake. Tangu safari yake ya kutoka nchini Tanzania, alivyopelekwa nchini Italia. Mambo aliyayoyapitia huko. Na lengo la kurudi lilikuwa ni lipi. Pia, Maya alimuomba radhi Benard na kumwambia kuwa, yeye ndiye chanzo cha kufukuzwa kazi. Kwani usiku ule, ulikuwa ni usiku aliokwenda kumuua bosi wake.

Bosi huyo alikuwa ni mmoja ya walioshiriki kuiingiza familia yao matatizoni.

Benard alisikitika. Akasema hakuna la kurekebisha kati ya kwani tayari yameshatokea. Maji yaliyomwagika, hufutwa tu. Hayarejesheki chomboni.

Maya akamshika mkono mvulana huyu. Akamweleza kuwa huo sio mwisho wa kitabu chao, bali ni mwanzo wa yote. Akamuomba awe kaka yake na wasaidiane kwenye mengi.

Benard alikubali. Binti huyu alikuwa na kesho nzuri sana kwenye maelezo yake. Akashirikiana naye mengi. Hata lile kusubiri siku ya kukutana na Inspekta na kumpeleka kwa mama yake. Nalo pia walilipanga.

Kama Kashmiri Kashmiri kwenda kwa Bibi Mboga, akakutana na kijana muokota makopo alihesabu ni jambo la bahati, basi afute mawazo hayo kokote huko alikokuwa.

Na sasa Maya yupo uraiani. Mama amelala. Akaamua kuketi na kaka wa hiyari kuingia naye katika mazungumzo. Binti huyu akalitamka jambo la hatari. Hatari ya kuyagharimu maisha yake. Benard aligoma. Hakuliridhia. Maya akawa katika msimamo. Akahitimisha kuwa, mtu wa kumzuia ama kumkubalia ni mama yake, hivyo yuko pale kusubiri ruhusa au katazo lake.

# 18

"Kwanini umeamua hivyo?" Swali lilimtoka Benard akihoji sababu ya uamuzi wa Maya.
Baada ya ukimya mdogo wa kutafakari, kama ilivyo kawaida yake, Maya alijibu, "Inspekta Kashmiri amechukuliwa na El Madame, sijui amempeleka wapi. Acha nilimalize hili mwenyewe."
Benard alimsikiliza huku akimtazama binti huyu macho yake. Yalibadilika rangi na kuwa mekundu. Akagundua kuwa hali sio nzuri na Maya yumo ndani ya hisia kali.
Ilikuwa ni mara ya pili Benard kumshuhudia Maya akiwa kwenye hali hiyo. Ya awali ni siku aliyokuwa akimuaga mama yake na kusema anakwenda kujikamatisha katika mikono ya polisi. Pale mama mtu alipokuwa akimwaga machozi kumzuia binti yake asijikamatishe na kwenda kukiri makosa yake, macho ya Maya yalibadilika na kuwa mekundu. Leo hali ileile imejirejea! Mbele ya maamuzi magumu!

"Nadhani sina muda pia wa kumsubiri mama aamke. Naweza kukuachia kazi?"

Benard akapandisha kichwa juu na kukishusha kuashiria yu-tayari.

"Utamlinda mama ikiwa sitarudi hai. Walau afie katika mikono yako. Natamani mzazi wangu roho yake itoke kwenye mikono ya mtu mwema. Benard, wewe ni mtu mwema. Haikuwa hivyo kwa baba yangu, sitamani iwe kwa mama!" Maya aliongea hayo huku akiwa wima.

Benard anafahamu msichana huyu. Anapoamua lake, si wa kupingwa, si wa kuzuiwa.

Wakaagana. Maya alipougeuza uso wake mbali, alipangusa machozi yaliyokuwa yameanza kumtiririka.

Akaondoka huku kiu ya kisasi kwa ajili ya familia yake ikiwa kubwa ndani mwake. Alikuwa akijitoa muhanga. Alikuwa akifanya mambo ya kugharimu uhai wake ili haki ipatikane.

Roho tano tayari zilishapotea katika mikono yake. Ikitangulia ile ya mjumbe wa mtaa, huyu alipokea kibano cha maana kuwataja wengine waliohusika. Akawaorodhesha akiamini ingekuwa ndiyo salama yake. Mwisho kabisa Maya akaporomoka na roho yake.

Wa pili, alikuwa ni mwenyekiti wa serikali ya mtaa wao. Yeye alipunguziwa muda wa mateso. Tayari alikuwa kwenye orodha ya wanaokistahili kifo. Alikabwa, uhai ukamchomoka akiwa kwenye kiti cha ofisi yake. Wengine watatu, wakiwa ni askari polisi. Ambao, kwa tamaa zao na kushindwa kuzishikilia ahadi walizoziweka wakati wanaingia kwenye utumishi wao, wakazama kwenye tamaa za matumbo yao. Wote walikutwa wamefariki kwa visu kukitwa katika shingo zao. Kifo cha aina moja. Walisalia watu wawili. Gwaya, ambaye tayari aliuwawa lakini Maya hakuwa akifahamu. Na mwingine mmoja. Huyu alikuwa mgumu zaidi. Tangu mwanzo, katika mipango yake, Maya alidhamiria kumfuata kupitia msaada wa Inspekta Kashmiri Kashmiri. Na sasa yu mpweke, anapaswa kumwendea akiwa mwenyewe. Isingekuwa kazi nyepesi.

*******

Tayari alishakula makofi kumi ya uso. Makofi makali. Akamwagiwa maji ya baridi mwili mzima, ya baridi

haswa, akaambiwa hayo yalikuwa ni mateso mepesi zaidi ya yote ambayo mtoaji aliwahi kuyatoa katika maisha yake.

Alielezwa aitazame simu yake kama mkombozi wake pekee. Simu ambayo mwanamke aliyekuwa amemteka, aliizima baada ya kuona ilikuwa ikiita bila mapumziko.

"Uko tayari?" Mwanamke akahoji.

Jamaa aliyekuwa hoi kitini, miguu na mikono imefungwa, alijibu kwa kutikisa kichwa.

"Kama kuna vitu ambavyo nimewahi kuvichukia hapa duniani, nikwambie kabisa, kinara wa mjumuiko wote ni ahadi za uongo. Napenda mtu anaposema kitu awe anamaanisha. Inspekta, narudia kwa mara ya pili na mwisho. Uko tayari?"

"Ndiyo," Inspekta Kashmiri akajibu huku sauti ikimtoka kwa tabu.

"Okay, tunapiga simu kituoni. Kituoni kwako. Nakuhitaji uwaulize Maya alipo. Kama wanaye, waseme watatuletea wapi, na mimi nitawakabidhi wewe. Tutabadilishana!" El Madame alitaka yote hayo yazungumzwe na Inpekta Kashmiri Kashmiri

mwenyewe. Alikuwa akipiga chenga ya kijasusi. Kuongea kwenye simu kwa sauti yako binafsi, tena kwa kuwapigia polisi, ni kujiingiza kwenye mtego wa kutambulika.

Majasusi hutumika vibadili sauti, au huwapa watu wengine kufikisha ujumbe wao.

Simu ikapigwa. Huko kituoni ikapokelewa. Mpigaji alipojitambulisha tu kuwa ni Inspekta Kashmiri Kashmiri, polisi wakampa umakini. Wakawa wenye kumuhoji yuko wapi.

Ni aheri hao polisi huko waliko, wangeuliza kuhusu mambo mengine yote, hata yale yasiyohusu. Kuliko lile swali moja, ambalo, ama liliwatoka kwa makusudi au kuwaponyoka...

Maya yuko wapi?

Waliposaili tu hivyo, El Madame alimpokonya haraka Kashmiri Kashmiri simu na kuizima hapohapo...

Aliyepokwa akabaki katika mshangao, bado hakuwa amemaliza kazi aliyotumwa...

"Mpaka hapa, inatosha!" El Madame alidai kazi imekamilika.

Ingehitaji akili ya ziada, yenye kujua namna ya kutafakari kwa kina, kama yake, kuelewa kwanini amesema kazi imekwisha na hajajua Maya alipo...

Ni kwamba, kama polisi wenyewe wanauliza kwa Inspekta Kashmiri Kashmiri Maya alipo, ina maana tayari ameshatoroka.

Hii haikuwa habari njema kwa El-Madame, akaipiga meza kuu kuu aliyokuwa ameigemea utasema ndiyo iliyojitambusha kwake ni Maya.

"Shit!" Tusi jipesi kutamkika na zito kimaana..

"Inspekta, nikuue kwa bunduki, au kwa kisu—nikunje?" Kisha akamuongelesha mateka wake ambaye hakujibu lolote.

Ingekuwa ngumu kwa mtu wa kawaida kuchagua lolote.

Kipindi El Madame akiwa katika kona ya kukaribia kukubali kushindwa, ikawa zamu ya simu yake kuita.

"Leo ni anakwenda kumalizana na Katibu mkuu wa wizara ya madini ambaye awali alikuwa ni mkurugenzi wa halmashauri!" Sauti ilitoa maelezo, hakuwa akiifahamu. Ni mara kwanza kuisikia.

"Nani?" Ikabidi aulize.

"Maya!" Mtoa taatifa hakuwa na maelezo mengi. Alijibu hivyo na kukata simu.

# 19

"Ndugu mgeni rasmi, huyo anayepita mbele yako ni mwanafunzi bora katika somo la Hisabati!" Kauli hiyo ikafuatiwa na makofi ya pongezi, vifijo vikashamiri.

Mzungumzaji wa shughuli aliwataja kwa mtiririko wanafunzi waliofanya vizuri katika kila somo. Nao wakawa wenye kuchukua zawadi zao kwa kumpa mkono mgeni rasmi huku wakipiga na picha za ukumbusho.

Yalikuwa ni mahafali ya kidato cha nne. Mahafali ya hadhi ambayo kwa upekee wake, yalihamishwa na kutofanyika katika ukumbi wa shule, yakapelekwa kwenye ukumbi maarufu jijini Dar Es Salaam. Na zile sababu kadhaa zilizotamkwa na mkuu wa shule hiyo zikisimama kama kinga. Ni basi tu, ipatikane hoja ya kuwafanya wazazi waingize mikono mifukoni mwao, watoe chochote kitu.

Kwa malipo yale ya ada yaliyokuwa yakikaribia milioni nne kwa mwaka, hakuwepo mzazi ambaye

alikishughulisha kinywa chake kuweka mkazo kuhusu mchango wa elfu hamsini ya ukumbi uliowekwa katika kadi!

Na kama yupo kati yao aliyejaribu walau kuwaza kutenga kiporo cha hoja, azma yake ingekufa, punde tu baada ya kumaliza kuisoma kadi hiyo na kukiona cheo cha mgeni rasmi. Katibu mkuu wa wizara ya madini!

Vinywa vya wengi vilienea tabasamu. Miziki ilichezwa, hotuba zikatolewa, risala ikasomwa na neno la aliyekuwa mgeni rasmi likapewa masikio....

Miongoni mwa masikio yote yaliyokuwemo mule, yalikuwemo masikio mawili yaliyokuwa yakilisikiliza neno hilo kwa hasira! Masikio haya yalihitaji nafasi ndogo tu, nafasi ndogo mno, kumfikia yule mzungumzaji na kumalizana naye. Ilikuwa ni sura ileile ya mkurugenzi wa halmashauri iliyoshiriki katika kuikandamiza familia ya haya 'masikio mawili'. Mkurugenzi aliyehamishwa majukumu na kugeuka katibu mkuu wa wizara nyeti kwa nchi. Na hakuna kingine kilichokuwa kikitafutwa zaidi ya kisasi.

Hatimaye muda wa chakula ukafika. Vikaingizwa 'vikokoteni' vidogo, vya kusukumwa, vyenye matairi, kwa juu vikiwa na makontena makubwa ya mabati yaliyo na vyakula. Makontena mengi. Yakasogezwa mpaka mbele.
Utaratibu wa chakula ukawa ni rahisi na wenye kuvutia.
Bado nawaza, ni nani huyo angethubutu kuihoji ile elfu hamsini ya ukumbi?
Ilianza meza kuu. Mgeni rasmi na wasaidizi wake. Nyuma ya mgeni rasmi kulikuwa na walinzi watatu. Wameshiba, hawa hawakuchukua sahani wala kubeba chakula. Jukumu lao lilikuwa ni kuhakikisha bosi wao yuko salama. Yote haya, bado tu yalikuwa yakishuhudiwa na kupigiwa hesabu kali na yale 'masikio mawili'...
Mwalimu mkuu alikuwa makini mno kuhakikisha wazazi wanafurahi, baada ya wageni wa meza kuu kuchukua chakula, akawataka wazazi wafuate. Hapa wakapatikana waliogoma. Hoja ikiwa wazingatiwe kwanza watoto. Wao nd'o wenye shughuli. Mdomo

wa mzungumzaji ukabadili upepo ulipokifikia kipaza sauti...
"Haya, wanafunzi, taratibu kabisa kwa utulivu kabisa, hayaa... Mnaweza kuja kuchukua chakula, tutaanza na mstari huu hapa! Mnaweza mkainuka, kuja..."
Mstari wa pili baada ya huo uliokuwa umeinuliwa, ulikuwa ni mstari ulioketi yale 'masikio mawili'.
Pindi 'masikio' haya yakiwa yameinuka baada ya ruhusa ya mstari wao kutolewa, alikuwepo mtu mwingine ndani ya ukumbi huohuo, ambaye hesabu zake zilikuwa kamili juu ya hayo 'masikio mawili'. Mtu huyo naye aliinuka huku akijisema kwa sauti ya chini iliyojaa ghadhabu, "Maya, ngoja leo nikuonyeshe kuku na yai kipi kiliumbwa na kipi kilitagwa!"
Yalikuwa ni mawindo ya kimyakimya. Kila ambaye akichukuwa chakula, alikusanya vitu vya kutosha na kuondoka kwenda kuketi. Hayakuwa kwa yale 'masikio mawili' ya Maya. Yeye alikumbatia sahani, na kisu, hakuchukua uma kama walivyofanya wenzake. Akasogea mpaka usawa wa meza kubwa. Badala ya kukunja kurudi vilipo viti... Akachupa na kuifikia ilipo

meza kuu. Lilikuwa ni tukio ambalo kwa mwanzo wake lilihesabika kama kioja. Wakawepo walioweza kucheka. 'Hii shule nayo kwa sapraizi! Muda wa maigizo umekwisha bwana. Fanyeni tule' Yupo mtu ambaye kauli hiyo ilimtoka kwa lawama.

Maya alikuwa juu ya meza. Wageni walihisi mwanafunzi. Walimu pia. Baadhi.

'Hata kama nd'o tukio la kiburudani nd'o upande juu ya meza ukanyage chakula cha mgeni rasmi?' Labda alikuwepo mwenye umakini ndani ya ukumbi huo akaweza kujiuliza swali la namna hiyo.

Walinzi waliokuwa nyuma ya mgeni rasmi, wakaisogeza ile miili yao iliyokuwa imeumuka kwa kubeba vyuma vizito na si mazoezi ya kimapigano. Binti akaokota sarakasi nyingine na kuwakuta, alichezea misuli midogo ilioyopo nyuma ya magoti, akauvunja ushirikiano katika ya mapaja na miguu. Ndani ya mapigo sita ya sekunde, wale walinzi watatu wote chini!

Bado kisu kilikuwa mkononi mwa Maya. Akakirusha kikaenda kukita kwa Katibu mkuu ambaye alikuwa akikimbia. Damu zikawa mgeni mpya katika tukio

ambalo umati ulikuwa umeanza kulichukua kwa simu zao kwa ajili ya ukumbusho. Damu ziliwaeleza kwa utulivu kabisa....

"Jamani eeeenh! Hakuna maigizo hapa. Watu wanapigika kweli!"

Mara, El Madame naye huyo!

Akasimama mbele ya Maya. Walitazamana mithili ya nyati walio ndani ya hasira kali. Maya akawahi kisu pembeni.

Ukumbi ulishaingia kwenye purukushani za sintofahamu. Wapo ambao hawakuingia hofu na kuendeleea kuamini haya ni maigizo. Na walikuwa wengi.

Kwa mtindo uleule wa urushaji, Maya alikifyatua kisu kumuelekea El Madame, kisu kikadakwa. Ikawa zamu ya El Madame sasa kumuonesha binti mdogo namna mashambulizi hutumwa...

Mlio wa risasi ukawawahi. Bunduki ilisikika. Polisi walifika eneo la tukio. Maya akakimbilia na kujichanganya katika ule umati wa watu waliohudhuria eneo hilo.

Wale waliokuwa wamo katika dimbwi la kuamini ule ni utani, sahani za vyakula vyao zilibinuka juu chini na vyakula kulambwa na sakafu.

Mwalimu mkuu aliyekuwa shuhuda wa karibu kabisa, tayari alishaweza kusota kwa makalio kujisogeza kwenye eneo alilokuwa akiamini salama ipo...

Shilingi chache za dhulma zimemleta katika kiama chake cha dunia. Hizo toba alizokuwa akizimwaga hapo, sitaweza kumaliza kuzisimulia!

# 20

SHUGHULI nzima ilishavurugika. Kila mmoja pale ukumbini alipiga kelele za aina yake alizokuwa akiamini zingeweza kumpatia msaada. El Madame alishanaswa katika uga wa sumaku ya dola. Polisi wenye bunduki walimzunguka. Mkononi ameshika kisu pekee. Maya hajulikani alipokimbilia.

"Weka chini silaha yako, laa si'vyo tunakupiga risasi!" Alikaripiwa.

Hakutii. Alijijua. Alijitambua kuwa yeye ni mtu mwenye hatia. Kujisalimisha ingekuwa ndiyo kujizamisha mazima. Asingesalimika mbele ya sheria.

Ubongo wake ukamshawishi afanye jukumu la kujiokoa. Akapanga ajinasue kwa kumuwahi askari mmoja ili amuweke kizuizini na atishie kutokusogelewa.

Hatua moja mbele tu kuifuata akili hiyo....

Paaaah!

Mlio wa risasi ukasikika. Watu waliokuwa wamejitupa chini wakalipuka kwa mara nyingine! Woga!

Wale waliokuwa na imani thabiti wakataja mpaka majina ya mababu zao katikati ya maandiko ya kidini, wenye hofu iliyopitiliza, sehemu zao za kutoa haja hazikuweza kusubiri mpaka muda ambao wangeweza kufika chooni. Kwa kiwango cha sauti ile, kila mmoja alikuwa akihisi risasi imepita kando ya tundu la sikio lake.

El Madame alikuwa chini. Jeraha katika paji la uso. Alishindwa kufuata angalizo alilokuwa amepatiwa. Imemgharimu uhai. Kisheria, hapo polisi alikuwa ametenda jambo la kupongezwa.

'Katika jitihada za kutaka kudhuru, akapigwa risasi ya kumtuliza!'

Risasi ya kumtuliza, nd'o kichwani kwake?

Maswali ya namna hiyo huwa hakuna wa kuthubutu kuyauliza!

Sasa ikawa ni zamu ya Maya aliyekuwa amekimbilia pasipojulikana...

Ulikuwa ni ukumbi mkubwa, wenye hadhi. Ukumbi wenye vyumba vingi kwa ndani. Chumba ya hifadhi ya

dharura. Chumba cha mgeni rasmi. Inapotokea anahitaji kujipanga kabla ya kuingia ukumbini. Na vinginevyo. Yakiwemo maliwato. Kote huko kulifanyika msako. Maya hakupatikana.
Kaelekea wapi?
Askari walijiuliza. Isingekuwa wepesi binti huyo kuweza kutoka nje. Tayari vikosi vya polisi viliuzunguka ukumbi wote na iliwekwa amri ya mtu kutokutoka.
Maya yuko wapi Maya?
Ndani ya dakika kumi za kulizungusha swali hili katika vichwa vya wengi ndani ya ukumbi ule, ikajongea akili iliyokuwa ikimfahamu Maya vilivyo, kuliko akili yoyote ile.
Muite 'Detective Benard Jolisa Papaliko! Hakupenda jina lake lipungumzwe hata herufi moja unapothubutu kulitamka ndani ya mazingira ya kazi.
Wakati Maya alipokuwa akifikiri mipango na maarifa yake yako mbele kwa hatua kumi, tayari begani mwake alikuwepo mtu aliyekuwa akiuchora mtikisiko wowote ambao angeufanya. Alikuwa ni yuleyule kijana aitwaye Benard. Kukutana kwao ilikuwa ni kama

sadfa tu, haikupangwa, lakini matokeo ya makutano hayo ndiyo yaliamua muendelezo.

Benard ni askari mpelelezi. Mzoefu mwenye kuyajua majukumu yake kwa mipaka na matakwa yote. Alitumwa na serikali kwa yule tajiri ili ampeleleze. Chini ya majukumu yenye 'kifuniko' cha ulinzi na mfanyakazi wa ndani. 'Shamba boy'.

Akiwa ndani ya mwendelezo wa kufanya kazi zake kwa utaratibu, bila ya pupa, anakutana na binti ambaye aliwahi kumtendea wema wa kumsaidia usafiri kutoka uwanja wa ndege mpaka maeneo ya karibu na Magomeni mapima. Ni aheri wangekutana tu, anakutana naye katika usiku uliotokea mauaji.

Hapo, uelekeo wa upelelezi wake ukabadilika, akatakiwa aingie kwenye jukumu jipya la kumchunguza Maya.

Aanzie wapi?

Akazama kwenye gereji iliyopo Magomeni mapipa. Mitaa aliyoishuku binti huyo kuishi. Akaweka kambi hapo, akitega mazingira ya kumchorea ramani binti na kumfahamu ni nani hasa. Ikibidi kujua, ikiwa amehusika, ama hajahusika kwenye yale mauaji.

Benard anafanikiwa kukutana na Maya. Kwa makusudi kabisa. Wala haikuwa bahati. Alijipanga kwa hilo.

La kushangaza, binti huyo akaonekana kumuamini. Akamueleza mipango mingi. Benard aliipokea. Kinywa chake kikijaa uongo uliopitiliza. Kuwa ni kijana aliye mjini bila msaada.

Kwa makali ya akili aliyokuwa ameisoma kuwa ipo kwa binti huyu, bado Benard alichagua kubaki kwenye mstari uleule aliouzoea. Utulivu.

Akishirikiana naye kwenye mengi na kuigiza si mwenye kuelewa chochote kwa undani. Siku zimesonga.

Maya akihisi yuko kwenye dhiraa moja kuzimaliza mbio, Benard tayari alikuwa ameshaugusa utepe wa hitimisho.

Ni yeye ndiye aliyempigia simu El Madame. Namba akiwa amechukua katika simu ya Inspekta wa polisi aliyekubali kufanya kazi kwa hisia binafsi, Inspekta Kashmiri Kashmiri. Ilikuwa ni simu moja tu, kwa kijana wa kitengo maalumu cha mawasiliano cha kipelelezi, taarifa zote zilizomo kwenye simu ya Kashimiri Kashmiri zilipatikana, hata namba ya El Madame.

Na lengo la kuwafanya wawili hao wakutane: Maya na El Madame, ni kuwaua ndege wawili kwa jiwe moja. Tayari ndege mmoja alibisha hodi katika lango la umauti. Ndege wa pili hajulikani alipo. Maya.
Yuko wapi?
Ubongo wa Benard ukaingia kazini. Detective Benard Jolisa Papaliko. Kama ambavyo alifurahia kuitwa. Amri kuu tatu zikatolewa ndani ya ukumbi ule. Ukiongeza ile ya 'hakuna mtu kutoka', zikawa nne.
Hii ikabadishwa, ikawa 'hakuna mtu kuingia'. Bado, zilibaki nne vilevile!

*******

Ndani ya ukumbi kulikuwa na makundi matatu ya watu. Hiyo ilikuwa ni hatua ya kwanza ambayo Mpelelezi Benard aliitumia. Kutambua aina ya watu waliomo katika eneo la tukio. Kulikuwemo wanaume, wanawake na watoto. Askari polisi hakuwajumuisha. Hakutenga vyeo, wala hadhi. Mbele ya hatari, binadamu wote hupaswa kuwekwa katika mzani mmoja.

Amri ya kwanza, wanaume waanze kutoka ukumbini. Kisha ukaguzi ufanyike kwa kila anayetoka.
Ya pili ikawa ni awamu ya wanawake. Hawa Benard aliagiza wapekuliwe mpaka mikoba waliyokuwa wameibeba. Bila kujali ni mikubwa ama midogo kiasi gani. Kwani Maya ni binadamu hatari anayeweza kujikunja hata kufika udogo wa pipi.
Alizungumza hilo kuonesha ni kwa namna gani huyo aliyekuwa akitafutwa ni kiumbe asiyekadirika.
Kundi la mwisho, likawa watoto. Kabla ya ukaguzi na kuruhusiwa kutoka. Askari wakapewa onyo na Benard. Wakaelezwa kuwa, Maya hajachagua kujificha kwa bahati mbaya. Bila shaka tayari alishapanga namna yake ya kutoroka. Na haipo nyingine zaidi ya kujifanya ni miongoni mwa wanafunzi kwani umri wake, umbile na muonekano vinaruhusu. Wakaombwa umakini. Ukaguzi uwe mara mbili zaidi.
Na wale wazazi waliotangulia nje, wanapaswa kusogea karibu, mara tu mtoto wanayemfahamu atatolewa nje, wamfuate. Yule ambaye atakuwa amekosa wazazi ama mlezi wa kumtendea hilo, ndiye Maya mwenyewe.

Akili ya Benard haikuwa ya kitoto. Hakika alistahili kuwa katika cheo kile cha kipelelezi.
Ili kupisha hekaheka hiyo na shughuli ifanyike kwa ustadi, yale makontena makubwa yakatolewa kwa kukokotwa na kuwekwa nje.
Ukaguzi ukaanza. Mwanafunzi mmoja mmoja. Hakubaguliwa wa kike, hakuachwa wa kiume. Ukumbi wa mahafali ukageuka kambi ya wakimbizi iliyo mpakani mwa nchi mbili zenye mtafaruku wa kisiasa.
Watoto wak'esha, hola! Maya hakuwekwa mkononi. Sasa hakukuwa na mwingine ukumbini. Pekua na pekua, pekua kwa kuchungulia mpaka matundu ya vyoo, geuza mpaka vitambaa vilivyotandikwa juu ya meza, pitisha pekesheni mpaka kwa askari wenyewe kwa wenyewe, Maya hayupo!
Amekwenda wapi?
Benard akiendelea kutafakari. Akizungusha hatua zake huku na huko akijutia muda aliotumia kumnasa binti huyo, alizidi kuvurugwa. Angekwenda kuwaeleza nini wakubwa wake waliomtuma?
Alijiona namna akifanana na Inspekta Kashmiri. Ambaye kwa muda huo aliswekwa ndani baada ya

kuokotwa kandokando mwa barabara. Aliwekwa ndani ili kujibu mashataka yaliyokuwa yakimkabili.
Kwamba na yeye ameshindwa? Akeshindwa kumuweka mikononi binti wa miaka kumi na sita? Binti mpaka amefanikiwa kumuua Katibu mkuu wa wizara, atakwenda kuwaeleza lipi viongozi?
Akakuna kichwa kufikiri kipi hakijatendeka. Kama wanaume, wote walikaguliwa, wanawake pia... Yakatolewa makontena....
Doh! Kufika hapo kwenye makontena hapo, kichwa chake kikapitisha moto kwa kasi sana! Makontena hayakukaguliwa!!! Yalitolewa tu.
Basi mkukumkuku, akiandamana na askari. Akafika mpaka nje yalipokuwa yamepelekwa. Yakaanza kufunuliwa moja baada ya lingine. La mchuzi, la nyama, la maharage, lenye mboga za majani, lilihofadhi pilau... Yote yalikuwa sawa.
Likafikiwa lililokuwa limebeba wali mweupe. Ikakutwa kasoro. Ikakutwa alama ya kiganja cha mkono. Kwamba, yupo mtu alikaa juu yake.
Benard akaishia kucheka huku akikuna kichwa chake. Kuteleza kidogo tu, nafasi finyu sana, Maya aliitumia.

Dakika hiyohiyo, simu yake ikawa yenye kuita..

"Najua utakuwa ukijiuliza nimeipata vipi namba yako wakati kwa kipindi chote hicho uliishi mbele yangu kama mtu usiye na simu..." Ilikuwa ni sauti ya Maya. Iliendelea, "Hata mimi nilijiuliza sana nilipokuachia kazi ya kumsubiri Inspekta. Ukaweza kumfahamu na kumfikisha kwa mama. Mtu wa kawaida, asiye na mafunzo, asingeweza kumjua kuwa ni Inspekta wa polisi. Waarabu wa Pemba hujuana kwa viremba. Huu msemo sikuusoma Ulaya Detective Benard Jolisa Papaliko! Niliujua hapahapa Tanzania. Niko njiani, nampeleka mama mbali na mikono yenu. Naahidi nitarudi kushughulika na wewe!!" Simu ya kutisha ikakatwa.

Mpelelezi Benard alipojaribu kuipiga tena, haikupatikana.

Maya alishaimaliza kazi yake, yeye amefeli. Na ameahidiwa kurejewa.

Alikuna kichwa kwa mara nyingine. Akaomba aletewe sahani kubwa, akapakua pilau, nyama na mboga za majani. Akaketi chini, ale.

Kama kwenye maisha yako hukuwahi kumuona mtu mwenye kushikwa na njaa ya ghafla, basi mtazame mpelelezi Benard.

**MWISHO!**